SIRI PART 3

JASUSI/GAIDI

SEASON 2

MTUNZI: PATRICK.CK



HADITHI HII NI MALI YA MWANDISHI NA HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA KWA HIYO HAIRUHUSIWI KUCHAPISHA, AU KUITUMIA KWA NAMNA NYINGINE HADITHI HII BILA RUHUSA YA MWANDISHI.HATUA KALI ITACHUKULIWA KWA YEYOTE ATAKAYEKIUKA MASHARTI HAYA..

SIMULIZI NYINGINE ZA MTUNZI PATRICK.CK

1.MISS TANZANIA
2.I WAS WRONG
3.TEN CHAPTERS
4.I DO
5.SERENA
6.BEFORE I DIE
7.BEYOND PAIN
8.PENIELA
9.QUEEN MONICA
10.THE FOOTBALL
11.I DIED TO SAVE PRESIDENT
12.KIAPO CHA JASUSI
13.KIKOSI CHA SIRI
14.SIRI

MAWASILIANO
0764294499

ILIPOISHIA SEHEMU ILIYOPITA

“Mathew kinachoendelea Afrika mashariki ni zaidi ya mapigano ya kidini.Yalianza mapigano ya makundi ya waumini wa dini na sasa yameibuka tena makundi mengine ya makabila,makundi ya kisiasa n.k.Suala hili limezidi kuwa pana zaidi kila uchao”

“Serikali za Afrika Mashariki zimefanya juhudi gani katika kumaliza vurugu hizo?akauliza Mathew

“Mathew machafuko ya kidini ni mabaya sana na kila siku yanaongezeka ukubwa na nguvu yake kama kimbunga.Majeshi yamelazimika kutumia nguvu kubwa na kilichotokea ni watu wengi kuuawa.Kwa ujumla hali ni mbaya sana Afrika Mashariki” akasema Habiba

“Ruby,Gosu Gosu,Austin.Wako salama kweli?akajiuliza Mathew

“Tuliweke na hilo pembeni nilitaka tu ufahamu kinachoendelea nyumbani.Kubwa zaidi

nililokuitia hapa ni kwamba kesho alfajiri tunasafiri mimi na wewe tunakwenda Marekani”

“Marekani?! Mathew akashangaa

“Ndiyo.Mbona umeshangaa?

“Nini tunakwenda kufanya huko? Akauliza Mathew

“Tunakwenda kuonana na wakuu wa IS”

“Wakuu wa IS wako Marekani? Akauliza Mathew na Habiba akatabasamu

“Mathew niliwahi kukwambia kwamba kuna

mengi bado huyafahamu unatakiwa ujifunze.Nitakueleza kidogo.” Akasema Habiba na kunyamaza kidogo halafu akasema

“Kundi la IS lilianzishwa na Marekani kama chombo cha kuwasaidia kuvamia nchi za kiarabu zenye utajiri wa mafuta na vile vile kuidhibiti nchi ya Iran isiweze kuwa taifa lenye nguvu zaidi katika eneo la Mashariki ya kati.Usishangae kusikia kwamba kundi la IS limeanzishwa na

Marekani.Yawezekana hufahamu lakini Mwaka 1970 shirika la ujasusi la marekani CIA lilikitumia kikundi cha Muslim Brotherhood cha Misri katika kuzuia Urusi isieneze sera zake katika nchi za kiarabu.Marekani pia waliunga mkono kundi la Sarekat dhidi ya Surkano nchini Indonesia,vile vile waliunga mkono kikundi cha Jamaat e Islami dhidi ya Zulfiqar Ali Bhutto nchini Pakistan.Hii ni historia fupi nimekupa utambue kwamba Marekani wamekuwa wakivisaidia

vikundi vinavyojihusiana na ugaidi pale inapolazimika kwa ajili ya maslahi yao.Tukiweka pembeni makundi hayo niliyokutajia tuje katika kundi la IS.Hili kundi ni zao la Marekani kama nilivyokueleza ambao wanatumia kundi hili kuvamia nchi maadui wa Marekani katika eneo la Mashariki ya kati,kulitumia kama kigezo cha kuvamia kijeshi nchi hasa zile zenye utajiri mkubwa wa mafuta na ndani ya Marekani wanatumia kundi hili kama tishio kwa usalama wa nchi hivyo

kuhalalisha udukuajiwa taarifa za wananchi kwa kigezo cha usalama.

Kwa muda mrefu sasa nimekuwa nikifahamika kama mfadhili mkuu wa kundi la IS na makundi mengine ya kigaidi lakini ukweli ni kwamba mimi ni chombo tu kinachotumika katika ufadhili huo bali wafadhili wakuu ni Marekani.Umewahi kujiuliza kwa nini sikamatwi japo ninafadhili ugaidi? Ni kwa sababu mimi ninatumika tu kama chombo.Mume wangu alikuwa anafanya hivyo na

alipofariki nilibeba mimi jukumu hilo.Wanaofahamu suala hili hata ndani ya Marekani ni watu wachache sana.Ninakwenda nawe kesho Marekani nataka ukajifunze kwani wewe ndiye utakayechukua mikoba baada yangu.Tutakaporejea safari hiyo nitakupa maelekezo nini kinafuata.Nadhani umenielewa Mathew.Ninakupa maelezo mafupi mafupi kukupa nafasi ya kujifunza.Jiandae kwa mambo makubwa yanayokuja huko

mbeleni” akasema Habiba Jawad.

Habiba alihitaji kupumzika hivyo hakutaka maongezi zaidi akamtaka Mathew naye akapumzike na kujiandaa kwa safari yao ya alfajiri.

Mathew alirejea chumbani kwake lakini kichwa chake kilikuwa kimevurugika kabisa

“Nina wasi wasi mkubwa na usalama wa Ruby kufuatia machafuko hayo makubwa yanayoendelea Afrika Mashariki.Ninatamani kumpigia simu lakini sitaki

ajue mahala nilipo” akawaza Mathew

“Abu kuna nini?Mbona sura yako imerudi tofauti na ulivyoondoka?Mama amekwambia nini?akauliza Najma

“Kesho tuna safari.Ninasikitika kukuacha peke yako” Mathew akadanganya

“Ouh mpenzi wangu kumbe ni hilo tu.Usipate taabu kwani mtarejea na utanikuta hapa ninakusubiri.Mama kakwambia mnakwenda wapi?

“Tunakwenda Marekani.Safari ya kibiashara”

“Mama anakuamini sana Abu Zalawi” akasema Najma na Mathew akachukua kitabu katika kabati lake akaitafuta namba ya simu ya Ruby akapiga lakini simu haikupatikana

“Hii inazidi kunipa wasi wasi kama Ruby ni mzima.Natamani niondoke hata sasa hivi niende Tanzania kujua kama yuko salama.Ruby ninampenda kwa moyo wangu wote na nilimuahidi kurudi nyumbani kwa ajili yak.....”

“Abu,huyu Ruby ni nani? Akauliza Najma.Mathew aliyekuwa ameelekeza macho ukutani akageuka na kustuka baada ya kumkuta Najma akiwa na kile kitabu chake ambacho ameandika mawasiliano ya watu mbali mbali

“Ruby ni Rafiki yangu” akasema Mathew na kuchukua kile kitabu akakifungia kabatini.

ENDELEA.....

DAR ES SALAAM – TANZANIA

Mataifa mbali mbali duniani yaliendelea kutoa wito kwa makundi ya kidini yanayopigana kuacha mara moja na kuitaka jumuiya ya kimataifa kuchukua hatua za haraka za kuzuia umwagikaji mkubwa wa damu unaoendelea katika eneo la Afrika Mashariki .Vikosi vya majeshi ya ulinzi vya nchi za Afrika mashariki vikisaidiana na vikosi vya jeshi la Marekani viliendelea na juhudi za

kudhibiti mapigano yale makubwa lakini pamoja na juhudi zao bado hali iliendelea kuwa mbaya.Mapigano yaliendelea kushika kasi kila uchao.Majengo mengi ya ibada na yale ya serikali pamoja na magari vilichomwa moto na makundi ya watu wanaopigana.

Nchini Tanzania mawasiliano ya simu na inteneti vilizimwa ili kuzuia watu kuwasiliana na kuhamasishana kushiriki katika vurugu.Ni taasisi muhimu tu za serikali ndizo

zilizoendelea kuwa na mawasiliano.Licha ya kutokuwepo kwa mawasiliano ya simu,bado vurugu ziliendelea na kuilazimu serikali kuongeza ulinzi zaidi katika sehemu muhimu kama vile mahospitali,mitambo ya kuzalisha umeme,mitambo ya kusukuma na kusambaza maji,mabenki na vituo vya polisi ambako makundi ya watu walikuwa wakivamia na kupora silaha ambazo walizitumia katika mapigano.

Saa tano na dakika kumi za usiku,Rais Dr Fabian

alimaliza kikao na wakuu wa vyombo vya usalama kikao kilichoanza saa kumi na mbili za jioni.Kwa muda wa siku nzima Dr Fabian amekuwa akifanya kikao baada ya kingine katika kujaribu kutafuta suluhu ya machafuko yale.Baada ya kumaliza kikao na wakuu wale wa vyombo vya ulinzi na usalama akawa na mazungumo ya faragha na mkuu wa majeshi kwa takribani dakika arobaini na walipomaliza akataarifiwa kwamba wakuu wa idara ya SNSA walikuwa wanamsubiri

kwa ajili ya kuzungumza naye.Rais akaelekeza wapelekwe nyumbani kwake ataenda kukutana nao huko kwani bado alikuwa na mazungumzo ya faragha na mkuu wa idara ya usalama wa taifa.

Saa saba kasoro dakika tisa Rais akaingia sebuleni kwake ambako aliwakuta Ruby na Gosu Gosu wakimsubiri.

“Samahani sana vijana wangu kwa kusubiri muda mrefu” akasema Dr Fabian

“Usijali mheshimiwa Rais,tunaelewa uzito wa

majukumu uliyonayo” akasema Ruby

“Sikuwajumuisha katika kikao cha wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuwa idara yenu ni ya siri na kazi zake zinafanywa kwa usiri mkubwa hivyo msijisikie kutengwa” akasema Dr Fabian huku akilegeza tai yake

“Tunaelewa mheshimiwa Rais” akajibu Ruby

“Kama hamtajali naomba tukapate chakula kwani hivi mnionavyo sijala chakula toka nilipokunywa chai asubuhi” akasema Dr Fabian na

kuongozana na akina Ruby katika chumba cha chakula.

“Vijana wangu urais ni mgumu sana.Nawashangaa wale wanaong’ang’ania madarakani.Sijamaliza hata kipindi changu kimoja cha urais lakini tayari nimeanza kufikiria kutowania kuteuliwa tena kipindi cha pili.Urais ni mzigo mzito.Tazama hivi sasa nchi imeingia katika machafuko na watu wote wananitazama mimi.Nimeubeba mzigo mzito mabegani mwangu kana kwamba mimi ndiye

niliyeanzisha hizi vurugu.Toka asubuhi sijapata hata nafasi ya kupumzika ni kikao baada ya kikao” akasema Dr Fabian

“Pole sana mheshimiwa Rais.Ni kweli umebeba mzigo mzito sana” akasema Ruby

“Tuachane na hayo.Mnaendeleaje upande wenu? Akauliza Dr Fabian

“Tunashukuru Mungu tuko salama na tunashukuru pia miundo mbinu yetu pia iko salama.Jengo letu kuwa karibu na ikulu imesaidia sana kwa machafuko kutofika huku” akasema Ruby

“Wafanyakazi wenu wote wako salama? Akauliza Rais

“Ndiyo mheshmiwa Rais wote wako salama.Tumeweka kambi pale pale katika jengo letu na sote tuko hapo hadi pale hali ya amani itakapokuwa nzuri” akasema Ruby na ukimya mfupi ukapita

“Jioni ya leo nimezungumza na Rais wa Marekani akanitaka tusitumie nguvu kubwa katika kutawanya makundi ya wanaopigana.Anadai idadi ya watu wanaouawa na vikosi vya ulinzi imekuwa kubwa hivyo

kuchochea machafuko zaidi.Si yeye tu bali hata umoja wa ulaya umetaka hivyo” akasema Dr Fabian na kunyamaza akaendelea kula halafu akasema

“Nawashangaa sana hawa viongozi wanaodai tusitumie nguvu kubwa.Yawezekana hawajawahi kukutana na machafuko kama haya ya kidini katika nchi zao ndiyo maana inakuwa rahisi kudai isitumike nguvu.Watu wanavamia majengo ya serikali,wanachoma majengo ya

ibada,wanapora,wanaharibu magari,wanachoma makazi ya watu,wanaharibu miundo mbinu halafu tusitume nguvu kuwazuia?? Akauliza kwa ukali

“Huu ni upuuzi mkubwa sana.Lazima tutumie nguvu kuzuia machafuko haya yasiendelee.Wanauawa watu wasio na hatia.Wanawake na watoto ndio wanaopata taabu kubwa katika machafuko haya.Tanzania tumezoea kupokea wakimbizi kutoka nchi nyingine lakini na sisi yametukuta,hatuna kwa kukimbilia.Tumeichezea

amani yetu na sasa tunayaona madhara yake ! Naapa kuendelea kutumia nguvu kubwa kuhakikisha haya makundi yanayochafua amani yetu yanafutiliwa mbali ! akasema Dr Fabian na kuweka kijiko chini hakuwa tena na hamu ya kula chakula.Alizama katika mawazo

“Mheshimiwa Rais” akasema Ruby

“Suala hili linanikosesha amani kabisa.Malizeni kula twende katika mazungumzo” akasema Dr Fabian.Ruby na Gosu Gosu walimaliza kula Dr

Fabian akawachukua wakaenda katika chumba cha mapumziko

“Ni saa tisa sasa mapambazuko yanakaribia.Toka mapambazuko ya jana sijafumba jicho na ninawataka ninyi wasaidizi wangu nanyi pia msifumbe macho yenu hadi pale tutakapohakikisha balaa hili limepita” akasema Dr Fabian halafu ukapita ukimya

“Vijana wangu nimefurahi kuwaoneni tena mkiwa salama.Nataka kufahamu kile

kinachoendelea ndani ya SNSA kwani toka zilipoanza vurugu sijapata wasaa wa kukaa nanyi tukazungumza yale yanayoendelea katika idara yenu.Vyombo vyote vya ulinzi na usalama kuanzia jeshi polisi,jeshi la wananchi,zimamoto na vingine vyote mnavyovifahamu wamejielekeza katika kudhibiti vurugu lakini mpaka sasa hakujakuwa na mafanikio yoyote vurugu bado zimeshika kasi" akasema Dr Fabian

"Mheshimiwa Rais idara yetu kama ilivyo jina lake

haijihusishi sana na masuala ya udhibiti wa vurugu kwani hiyo ni kazi ya jeshi la polisi lakini katika suala hili sisi tumejikita zaidi katika kufahamu chanzo cha hizi vurugu ni nini au ni nani? Japo vurugu hizi zinatufanya tushindwe kufanikisha jukumu letu ipasavyo lakini kuna mambo kadhaa tumeyabaini.Katika uchunguzi wetu wa awali tumebaini kwamba vurugu hizi zinaweza kuwa ni zaidi ya tunavyofikiri.Yawezekana

ikawa ni zaidi ya chuki za kidini”

“Kwa nini unasema hivyo?Kuna kitu mmekigundua? Akauliza Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais,kuna chembe chembe za siasa ndani ya vurugu hizi” akasema Ruby halafu akanyamaza kidogo

“Muda mfupi baada ya mkuu wa jeshi la polisi kutoa tamko akiwa jijini Tanga kuwataka watu waendelee kuwa wavumilivu na kwamba serikali inayafanyia uchunguzi matukio yale ya mauaji ya

viongozi wa dini yaliyokuwa yanaendelea jijini Tanga,katika ukurasa wake wa twitter Karim Abdallah ambaye anaongoza chama cha siasa cha TPD aliandika ujumbe akiwahimiza waumini wa dini ya kiislamu jijini Tanga kwenda kuwatafuta wale ambao anadai walimuua Sheikh mkuu wa mkoa wa Tanga.Ujumbe huo wa kichochezi haukukaa sana akaufuta lakini tayari watu wengi walikwisha usoma kwani Karim ana watu wengi wanaomfuatilia katika mitandao ya kijamii.Kwa

mwanasiasa kama huyu kuandika ujumbe kama ule ambao una mlengo wa uchochezi inatupa wasiwasi na kutufanya tulione suala hili kama lina chembe chembe za siasa ndani yake.Ukichunguza katika vurugu hizi utaona kuna makundi yameibuka ambayo yanalenga katika kuharibu miundo mbinu muhimu vile vile kuvamia na kuharibu majengo ya taasisi za serikali”akasema Ruby na Dr Fabian akapandwa na hasira

“Namfahamu Yule kijana ni mwanasiasa mchonganishi

na amekuwa akiandika mara kadhaa jumbe za uongo na uchonganishi kati ya wananchi na serikali. Ruby kuna picha nimeanza kuipata kufuatia maelezo yako.Sikuwahi kuusoma huo ujumbe wa twitter aliouandika lakini naamini kabisa lazima Karim atakuwa na mahusiano na vurugu hizi.Kijana mshenzi sana Yule ! akasema kwa ukali Dr Fabian

“Aliufuta ujumbe huo ndani ya muda mfupi tu lakini wengi tayari walikwisha usoma” akasema Ruby

“Mmekwisha anza kumfanyia uchunguzi huyu jamaa??akauliza Dr Fabian akionekana kuwa na hasira kali

“Mheshimiwa Rais kuna ugumu kidogo katika kulitekeleza hilo.Kwanza tumeshindwa kufuatilia mawasiliano yake yote kwani hakuna mawasiliano ya simu wala intaneti.Pili ni ugumu wa kumfuatilia nyendo zake kwani huko mitaani kumetapakaa vurugu na magari yanachomwa.Barabara nyingi zina vizuizi vya kuzuia magari

hivyo tumepata ugumu katika kuifanya kazi yetu” akasema Ruby

“Mngenieleza mapema ili niangalie namna ya kuwawezesha kutekeleza majukumu yenu” akasema Dr Fabian

“Ndiyo maana tuko hapa mheshimiwa Rais kuleta maombi yetu kwako”

“Nini mnakihitaji Ruby?akauliza Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais kwa hivi sasa hakuna mawasiliano ya simu hapa nchini isipokuwa kwa ofisi nyeti za

serikali.Pamoja na kuzima mawasiliano ya simu kwa lengo la kuzuia watu kuhamasishana kushiriki katika vurugu,lakini bado haijasaidia sana kwani bado vurugu zinaendelea.Tunashauri mawasiliano ya simu yarejeshwe kama kawaida” akasema Ruby na Dr Fabian akaonyesha mstuko kidogo

“Turejeshe tena mawasiliano ya simu? Hali itakuwa mbaya zaidi kwani watu wanatumia simu kuwasiliana na kuhamasishana

kushiriki katika vurugu na hili ndilo lilipelekea tukaamua kuzima mawasiliano yote ya simu na intaneti na hii itaendelea hivi hivi hadi pale vurugu zitakapokoma kwani tukirejesha mawasiliano tutaendelea kuongeza chuki na vurugu zitapamba moto ! Akasema Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais pamoja na nia njema ya jambo hilo lakini kuna athari zake vile vile.Siku hizi watu wanategemea sana simu zao katika shughuli mbali mbali hivyo mkiwanyima fursa ya

kutumia simu zao ni kuwafanya maisha yao yawe magumu zaidi hata hivyo sababu kubwa ambayo tunashauri mawasiliano ya simu yarejeshwe kama kawaida ni ili kuwafanya watu waone maisha yamerejea kawaida wataamini kwamba hali ya amani imeanza kuboreka.Jambo lingine ni kwamba mamilioni ya watanzania sasa wanamiliki simu janja.Tutazitumia simu hizo kufikisha ujumbe kwa wananchi kuhusu umuhimu wa amani na kuepuka

kushiriki katika vurugu zinazoendelea hivi sasa.Mheshimiwa Rais utalihutubia taifa na ili ujumbe wako uweze kuwafikia watu wengi zaidi na kwa haraka tutatumia teknolojia ili hotuba yako iweze kutazamwa na watu wote wenye simu janja zao kwa mara moja”akasema Ruby

“Inawezekana? akauliza Dr Fabian

“Ndiyo mheshimiwa Rais inawezekana.Simu janja zote ambazo zitakuwa zimewashwa muda huo zitapokea hotuba yako moja kwa moja bila

mmiliki kujiunga sehemu yoyote.Kwa mfano waweza kuwa unawasiliana na mtu Fulani au unafanya chochote katika simu basi kila kitu kitasimama kwa muda na mtumiaji ataunganishwa moja kwa moja na hotuba ya Rais.Pale hotuba itakapokuwa imemalizika basi mawasiliano yao yataendelea kama kawaida na ujumbe utakuwa umewafikia karibu nusu ya nchi na hii inaweza ikasaidia sana kuwafanya watu wakatafakari kuhusu hizi vurugu na inaweza ikasaidia

zikapungua kama si kumalizika kabisa” akasema Ruby

“Hilo ni wazo zuri Ruby.Sikuwa nimelifikiria kabisa” akasema Dr Fabian

“Hilo linawezekana mheshimiwa Rais na itatusaidia hata sisi kupata nafasi nzuri ya kumfuatilia Karim kujua mienendo yake na kufahamu mahala alipona tutamchukua ili atueleze alichomaanisha katika ule ujumbe wake wa uchochezi” akasema Ruby

“Nimekuelewa Ruby na ahsante sana kwa wazo hili nitalifanyia kazi.Hilo jambo litatekelezwa kesho.” akasema Dr Fabian

“Baada ya hotuba yako hiyo unaweza ukawatafuta viongozi wa dini mkakaa meza moja kulijadili suala hili na mnaweza kujikuta mmepata muafaka kwani chanzo cha vurugu zote ni masuala ya kiimani” akasema Ruby

“Kuhusu hilo la kukutana na viongozi wa dini nilikuwa nafikiria kuwakamata viongozi wote wakuu wa dini na

kuwafungia sehemu moja niwaache wazungumze hadi muafaka upatikane.Tukifaulu kudhibiti makundi ya dini tutakuwa tumelimaliza suala hili kwani hayo makundi mengine ya waporaji yanajikinga na mwavuli wa machafuko ya kidini" akasema Dr Fabian

"Mheshimiwa Rais sidhani kama hiyo ni njia nzuri kwa sasa.Kuwakamata viongozi hao wa dini kwa sasa itakuwa ni kuongeza mafuta kwenye moto kwani chanzo cha vurugu hizo ni kuuawa kwa viongozi wa

kidini hivyo viongozi wengine wakikamatwa hata kama ni kwa nia njema basi vurugu hizi zitaongezeka mara mbili” akasema Ruby

“Ruby hawa viongozi wanaweza wakawa na mchango mkubwa sana katika kutafuta suluhu ya vurugu hizi.Umekuwa ni utamaduni wetu kukaa mezani kuzungumza kila pale kunapokuwa na tofauti zozote za kiimani naamini hata sasa kama wakikaa pamoja basi wanaweza wakazungumza wanaweza wakafikia

makubaliano na wakazungumza na waumini wao kuwasihi waache vurugu” akasema Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais,nasema haitakuwa rahisi kwa viongozi hao wa dini kuwa na maelewano hasa ukiangalia chanzo cha vurugu hizi.Ukiangalia namna vurugu hizi zilivyoanza hapa kwetu Tanzania ,aliuawa kiongozi mmoja wa kanisa na waumini wake kadhaa,usiku wa siku hiyo hiyo akauawa sheikh mkuu wa mkoa wa Tanga na hii ilipeleka kila upande

kulaumu watu wa imani nyingine kuhusika katika mauaji yale ya viongozi na vurugu zikaanzia hapo.Mbegu mbaya ya chuki tayari imekwisha pandwa miongoni mwa waumini na viongozi wao wa dini,kila upande ukiwachukia wengine.Hata ukiwaweka pamoja kila upande utalaumu upande mwingine kwamba ndio chanzo cha vurugu.Njia pekee ya kulitatua suala hili ni kutafuta chanzo cha vurugu ni nini au ni nani? Tunatakiwa kufahamu nani waliomuua

yule kiongozi wa kanisa na waliomuua Sheikh mkuu wa Tanga? Tukifanikiwa kuwafahamu watu hao basi tunaweza kupata mwanga wa vurugu hizi na hata ukiwakutanisha viongozi wa dini na ukawaeleza kuhusiana na hiki tunachokifanya wanaweza wakaelewa” akasema Ruby

“Papo hapo tusisahau kwamba vurugu hizi zilianza Uganda na kuenea Tanzania hadi Kenya.Tukitaka kupata kiini cha vurugu hizi tuanze kuchunguza namna

zilivyoanza nchini Uganda.Huu ni kama ugonjwa ambao umeibuka Uganda ukaingia Tanzania na Kenya na kama hakutakuwa na tiba ya haraka basi ugonjwa huu unaweza ukasambaa Afrika nzima” akasema Gosu Gosu

“Uko sahihi Gosu Gosu.Hali hii lazima idhibitiwe kwa gharama zozote.Hatuwezi kuacha hali hii ikaendelea.Nchi imesimama kutokana na vurugu hizi ambazo ni kubwa hadi kushindwa kudhibitiwa na vikosi vyetu vya

ulinzi.Wamekuja wanajeshi wa Marekani lakini bado hawatoshi.Vurugu ni kubwa” akasema Dr Fabian

“Mheshimiwa rais kwa nini Marekani imetuma wanajeshi wake Afrika mashariki? Uliomba msaada kwao? akauliza Ruby

“Sikuomba msaada wowote kutoka Marekani.Rais wa Marekani alilazimika kutuma wanajeshi kwa ajili ya kusaidia kuimarisha hali ya amani vile vile kulinda raia wa Marekani na wa nchi nyingine za kigeni waliokwama Afrika

mashariki vile vile kulinda balozi zake.Kama mnavyojua ubalozi wa Marekani nchini Uganda ulichomwa moto na watu katika vurugu hizi zinazoendelea hivyo wamechukua tahadhari katika balozi zao nyingine za Dar es salaam na Nairobi.Vile vile wanatusaidia katika ulinzi wa miundo mbinu muhimu kama vile bandari.Wameleta meli za kijeshi katika bandari za Dar es salaam na Tanga ambazo zinasaidia katika ulinzi wa bandari hizo.Huu ni msaada

mkubwa wametupa” akasema Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais,kubwa lililotuleta kwako ni hilo tulilokueleza kwamba mawasiliano ya simu yarejee kama kawaida ili kutuwezesha kufanya shughuli zetu kwa wepesi zaidi” akasema Ruby

“Hilo litafanyiwa kazi kesho msihofu lakini hakikisheni huyu kijana Karim anapatikana tena ikiwezekana achukuliwe ahifadhiwe katika moja ya nyumba zetu ateswe sana hadi aeleze alimaanisha nini kuhusiana na ujumbe huo

wa kichochezi aliouandika katika ukurasa wake wa twitter.Nataka huu uwe ni mwisho wa Karim ! akafoka DrFabian

“Tunalifanyia kazi hilo mheshimiwa Rais na tutafahamu kila kitu” akasema Ruby na kumtazama Gosu Gosu

“Mheshimiwa Rais umechoka sana naomba tukuache upumzike hata kidogo kwani inakaribia saa kumi na moja za alfajiri sasa” akasema Ruby

“Nitawezaje kulala wakati wananchi wangu hawajalala wanakesha kwa hofu na wengine wakiishi katika makambi kama wakimbizi ndani ya nchi yao kwa hofu ya usalama wao?Nitalala pale ambapo vurugu zitakoma.Kwa hivi sasa ninakwenda kuzungumza na Rais wa China katika simu.Nawashukuruni sana kwa mawazo mazuri mliyonipa.Nadhani hata wasaidizi wangu nao pia wamechanganyikiwa na haya yanayoendelea ndiyo maana hakuna hata mmoja wao

aliyenipa ushauri kama huu mlionipa ninyi.Nendeni mkaendelee na kazi muhakikishe watu wenu wote wanakuwa salama na vile vile muhakikishe mnawapata walioanzisha vurugu hizi" akasema Dr Fabian akaagana na akina Ruby wakaondoka kurejea katika jengo la ofisi yao ambalo halikuwa mbali na Ikulu.Toka vurugu zilipoanza,karibu wafanyakazi wote wa SNSA waliweka kambi hapo katika jengo la ofisi yao kwa ajili ya usalama wao.

“Gosu Gosu tuna kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha tunapata kiini cha vurugu hizi.Naamini hazikuibuka hivi hivi lazima wapo waliozianzisha.Ni akina nani na nini lengo lao? Hayo ndiyo maswali ambayo tunahitaji kuyatafutia majawabu” akasema Ruby

“Nyakati kama hizi ndipo humkumbuka sana Mathew Mulumbi.Naamini huko aliko anaona kile kinachoendelea hapa nchini.I miss him so much” akasema Gosu Gosu.

“Are you scared Papii?akauliza Ruby

“I’m not scared.Mimi ni mwanajeshi toka nikiwa mdogo nimeishi katikati ya mapigano makubwa hivyo sijawahi ogopa hata mara moja na sintoogopa kamwe” akasema Gosu Gosu

“Good.Mathew hayupo na jukumu hili ni letu.Tutamshirikisha pia Austin pale itakapolazimu.Tuna kazi kubwa ya kuhakikisha tunauchimba mzizi wa machafuko haya” akasema

Ruby na ukimya mfupi ukapita halafu Gosu Gosu akasema

“Ruby kuna kitu nataka kuuliza naomba tafadhali uwe mkweli” akasema Gosu Gosu

“Siku zote nimekuwa mkweli kwako.Uliza nitakujibu”

“Ni kuhusu Mathew.Wewe ndiye ulikuwa mtu wa mwisho kuonana naye.Unafahamu mahala alipo? akauliza Gosu Gosu.Ruby hakujibu akaendelea kuendesha gari.Usiku huu hakuwa na dereva yeye ndiye aliyeshika usukani.

“Nijibu Ruby.Unafahamu mahala alipo?

“Kwa nini unahitaji kujua Gosu Gosu?

“Mathew ni kaka yangu,ni mtu wangu wa karibu.Nilipofumbua macho na kumuona sikuamini macho yangu kama kweli ni yeye.Nilidhani labda ni mzimu ninauona.Kumbe siku zote hisia zangu kwamba hakuwa amefariki ni za kweli.Kwa bahati mbaya nilipata muda mfupi sana wa kuwa naye kisha akatoweka tena na sijafahamu alikuwa wapi,nini

kilimtokea na amekwenda wapi.Nahitaji kufahamu kama kuna chochote alikwambia” akasema Gosu Gosu.Zikapita dakika mbili Ruby akasema

“Alinieleza kwa ufupi sana kuhusiana na mambo aliyoyapitia.Aliniambia kwamba alitekwa na Mossad na amepitia mateso mengi sana.Ukimtazama mgongo wake wote umejaa makovu mengi ukionyesha namna alivyopitia mateso makali.Alikuwa makini sana katika kueleza mahala alipokuwa.Kuhusu mahala

alipo sasa sifahamu na alinitaka atakapoondoka nisimtafute ila aliweka ahadi kwamba atarejea tena”akasema Ruby

“Hakukueleza anakwenda wapi? Akauliza Gosu Gosu

“Hapana hakunieleza na alinitaka nisijaribu kumtafuta lakini…….” Akasema Ruby na kunyamaza kidogo

“Kuna nini Ruby?

“Kuna kitu nilikigundua” akasema Ruby na kunyamaza tena.

“Katika kipindi chote alichorejea nilikuwa naye na

niligundua kuna mtu alikuwa anawasiliana naye na kumpa taarifa mbali mbali kuhusiana na operesheni ile iliyomalizika ya kumuua James Kasai”

“Alikuwa akiwasiliana na mtu? akauliza Gosu Gosu.

“Ndiyo kuna mtu alikuwa anawasiliana naye”

“Hukufanya uchunguzi kujua alikuwa anawasiliana nani?akauliza Gosu Gosu

“Hapana sikuchunguza.Mathew hapendi kuchunguzwa.Mtu huyo alikuwa anawasiliana naye usiku tu na alikuwa

anawasiliana naye akiwa amejifungia ofisini kwake hii ina maana kwamba hakutaka mimi au mtu yeyote kufahamu kuhusu mawasiliano yao na mimi sikutaka kuchunguza.Kila alipotoka kuwasiliana na mtu huyo alikuwa anakuja na taarifa mpya.Mathew ana siri kubwa sana anatembea nayo.Tufuate vile alivyoelekeza na muda utakapofika atarejea na atatuweka wazi nini kinaendelea katika maisha yake.Sisi ni ndugu zake na

hataweza kutuficha kitu” akasema Ruby

“Sawa Ruby nimekuelewa.Ahsante sana kwa kuwa muwazi” akasema Gosu Gosu

“Naamini umeridhika kwa haya niliyokueleza.Tunalifunga suala la Mathew hadi pale tutakaposikia chochote kutoka kwake kwa sasa tujielekeze katika kuuchimba mzizi wa hizi vurugu zinazoendelea” akasema Ruby.

Walifika katika jengo la ofisi yao kuu.Ni watu wachache tu waliokuwa ofisini

alfajiri hiyo wengi walikuwa katika mahema yaliyotengenezwa kwa ajili yao pembeni ya jengo la ofisi.

“Gosu Gosu tutumie muda huu mfupi uliosalia kabla ya mapambazuko tupumzike kwani tutakuwa na ratiba ndefu sana siku ya leo” akasema Ruby na kila mmoja akaelekea katika sehemu yake ya kulala

WASHINGTON DC – MAREKANI

Ni saa tatu za usiku jijni Washington DC Marekani.Katika ikulu ya Marekani Rais William Washington na makamu wake Mark Piller walimaliza kutazama hotuba ya Rais Armen Hijazi wa Iran.Ni hotuba iliyosubiriwa kwa hamu duniani,wengi wakitaka kusikia msimamo wa Iran kuhusiana na matamshi ya rais wa Marekani William Washington kwamba atalifuta taifa la Iran.Katika hotuba

yake hiyo ya kumjibu William Washington,Rais Armen Hijazi aliionya vikali Marekani kutothubutu kwa namna yoyote ile kuvamia ardhi ya Iran kwani watakachokipata kitaingia katika historia ya dunia.Kama haitoshi Rais Armen alimtaka Rais wa Marekani kufuta kauli yake kwamba atalifuta taifa la Iran kwani kauli yake hiyo ingeweza kumrudia yeye na taifa lake.Ilikuwa ni moja ya hotuba iliyoleta hofu kubwa kwa Marekani na dunia wakihofia kuzuka kwa vita

kubwa kwani Rais Armen aliweka wazi kwamba nchi yake iko tayari kwa vita na Marekani na alisistiza kwamba wataishambulia Marekani pamoja na washirika wake watakaoisaidia na alitishia kwamba baada ya vita hiyo Marekani haitakuwa sawa tena na itachukua zaidi ya miaka hamsini kuijenga tena Marekani.Katika kumalizia hotuba yake Rais Armen aliweka wazi mipango ya Iran ya kuendelea na urutubishaji wa madini ya Urani.

“Huu ni upuuzi mkubwa sana ! akafoka Rais William baada ya hotuba ile kumalizika

“Siwezi kuvumilia upuuzi kama huu.Armen hawezi kututamkia maneno kama haya sisi ! akaendelea kufoka William.

“Mheshimiwa Rais haya maneno yote aliyoyazungumza Armen ni upuuzi na ni maneno ya mtu aliyeshindwa.Iran haina uwezo wowote wa kuipiga Marekani”akasema Mark Piller

“Siwezi kuvumilia ujinga wa namna hii.Marekani ni

taifa kubwa na hatuwezi kukubali taifa kama Iran kututolea vitisho vya namna hii.Ninaapa lazima niishikishe adabu Iran ! akaendelea kufoka William ambaye ni mwepesi sana wa kupandwa na hasira

“Mheshimiwa Rais hiki alichokisema Armen kisikukoseshe amani.Hakuna anachoweza kufanya kwetu.Haya matamshi yake aliyoyatoa leo dhidi yetu hayatabadili mipango yetu dhidi ya taifa hilo lakini nashauri mheshimiwa Rais

huyu mtu tumuendee taratibu” akasema Mark Piller

“Kiburi alichokionyesha Armen hakiwezi kuvumilika.Ameongea kwa kujitapa kabisa kwamba nchi yake itaendelea na urutubishaji wa madini ya Urani.Hatuwezi kuiacha Iran ikaendelea na zoezi hili la urutubishaji wa madini ya Urani.Lazima tuchukue hatua kali sana dhidi ya taifa hilo ! akaendelea kufoka William Washington

“Mheshimiwa Rais suala hili si jepesi na tunahitaji

umakini mkubwa sana katika kulishughulikia.Armen ni Rais mjanja sana.Ametoa matamshi yale akitegemea kwamba Marekani lazima itahamaki na kuanza haraka kuchukua hatua.Lazima tuwe makini naye sana.Tumuonyeshe Arman kwamba sisi ni taifa kubwa na hatukurupuki”akaksema Mark Piller

“Mark hatuna muda wa kumbembeleza huyu mtu.Uvumilivu wangu umefika ukomo.Kinachofuata ni kumtandika vikali,kuharibu

vinu vyake vya nyuklia na kumuondoa madarakani rais Armen ! akasema William

“Mheshimiwa Rais,ni mapema sana kufikia hatua hiyo” akasema Mark lakini William aliyekuwa amewaka hasira akamgeukia akamtazama kwa macho makali na kusema

“Unataka huyu mtu aendelee kutoa vitsho kwa Marekani? Unadhani ni hofu ya namnagani wameipata watu wetu kufuatia matamshi yake ya kuivuruga Marekani? Katu hatuwezi kuwaacha wananchi

wetu waendelee kuishi kwa hofu ya vitisho vya Iran.Hawatatuelewa tutakaposhindwa kuchukua hatua zozote za kuwalinda.Msuguano huu na Iran umechukua muda mrefu na sasa umefika wakati wa kuumaliza.Niamini Mark ninakwenda kulimaliza suala hili .Siwezi kuipa nafasi Iran ya kuendelea kuruubisha madini ya Uran.Iran ikifanikiwa kutengeneza bomu la nyuklia hatutaweza kumdhibii tena na eneo lote la Mashariki ya kati litaingia katika hofu

kubwa.Lazima tuwahi angali mapema na njia pekee ni kuitandika kijeshi” akasema William

“Mheshimiwa Rais msuguano huu wa Marekani na Iran umechukua muda mrefu kwa sababu mpaka sasa hatufahamu Iran anamiliki silaha za namna gani.Mpaka sasa hatufahamu kwa nini Iran inakuwa na kiburi cha kutunishiana misuli ya kijeshi na Marekani.Hakuna taifa katika zama hizi ambalo limewahi kutamka kuishambulia Marekani zaidi

ya Iran.Lazima kuna kitu kinaipa kiburi Iran cha kuwa tayari kuingia vitani na Marekani hata kesho.Nimekuwa katika shirika la ujasusi CIA kwa muda mrefu na tumekuwa tukihangaika kujua Iran ina silaha gani kali lakini mpaka leo hatujafanikiwa kujua Iran anamiliki silaha gani.Iran wamekuwa wakidai kwamba wana makombora ya masafa marefu na wametishia kushambulia nchi zote washirika wa Marekani katika Mashariki ya kati ikiwemo

Israel.Mpaka sasa hatuna uhakika kama hiki wanachokisema ni cha kweli ndiyo maana nasema kwamba hatuwezi kukurupka katika suala hili.Tunao uwezo wa kumtandika Iran lakini ni vipi kama madai yake ya umiiki wa silaha kali ni ya kweli.Vile vile tukiivamia Iran kijeshi tutakuwa tumeanzisha mgogoro mwingine kwani Iran na Urusi wana urafiki mkubwa na wamekuwa wakisaidiana kijeshi.Hatutapigana vita na Iran pekee bali tutakuwa vitani na Urusi pia.Usisahau vile vile

kwamba hivi karibuni Rais wa Iran alifanya ziara nchini China na mahusiano ya Iran na China yameanza kuboreka hivyo nchi hizi lazima zitamuunga mkono Iran kama tutaishambulia kijeshi.Tazama namna Iran na Urusi walivyoshirikiana kuiunga mkono serikali ya Syria hadi kuiwezesha kukomboa asilimia zaidi ya tisini ya maeneo yaliyokuwa yanashikiliwa na waasi ambao tulikuwa tunawaunga mkono.Suala hili ni pana sana mheshimiwa Rais na inahitaji busara kubwa na

mikakati mizito katika kulishughulikia” akasema Mark Piller

“Mark kauli yako ni uoga.Siogopi kuipeleka nchi vitani ili kuisambaratisha Iran.Marekani si taifa la kutolewa vitisho na taifa dogo na dhaifu kama Iran !

“Mheshimiwa Rais ninazungumza kama kachero mbobezi.Kabla ya kufanya maamuzi yoyote tunahitaji kwanza kujiridhisha kuhusu uwezo wa Iran kijeshi na aina ya silaha ilizonazo.Tunahitaji kujiridhisha kuhusu madai

hayo ya Iran kuwa na makombora ya masafa marefu.Tunahitaji kujiridhisha kuhusu uwezo wake wa kutengeneza bomu la nyuklia.Tunahit……”

“Mark Piller ! akasema Rais William na kumkatisha Mark

“Umefanya kazi CIA karibu nusu ya umri wako na kwa muda huo wote mmekuwa mkihangaika kupata taarifa kuhusu mfumo wa makombora na silaha za Iran bila mafanikio.Itapita miaka mingapi ili tuweze kupata

taarifa hizo za silaha za Iran? Kama marais waliopita walivumilia mimi sina uvumilivu huo.Nataka nilimalize suala hili.Iran awe na makombora makubwa au madogo lazima atandikwe ! akaendelea kusisitiza William

“Mheshimiwa Rais kuna jambo muhimu naomba nikueleze” akasema Mark Piller

“Mark tunazungumzia suala la Iran na tutakapomaliza ndipo utanieleza hilo unalotaka kunieleza.Nataka mimi na

wewe tufike muafaka kwanza kuhusu suala hili la Iran kabla sijaomba ridhaa ya bunge !

“Mheshimiwa Rais ninachotaka kukwambia ni kuhusiana na suala hilo hilo la Iran” akasema Mark na Rais William aliyekuwa amesimama akaketi

“Nini unataka kunieleza?

“Nimekuwa nikiandaa mpango wa siri wa namna tutakavyoweza kulishughulikia suala hili la Iran” akasema Mark

“Unaandaa mpango wa siri ? Akauliza William akionekana kushangaa

“Ndiyo mheshimiwa Rais.Sikuwahi kukwambia suala hilo kwani maandalizi yake hayakuwa yamekamilika lakini kwa hapa tulipofika inabidi nikueleze ukweli ili mimi nawe tuwe katika ukurasa mmoja.”

“Nakusikiliza Mark” akasema William

“Kabla ya kukueleza kuhusu mpango huo kuna jambo ambalo nataka

ulifahamu ambalo naamini hulijui ila halitakufurahisha”

“Nini unataka kunieleza Mark? Akauliza William.Ukapita ukimya mfupi Mark akitafakari namna ya kuanza kumweleza Rais kisha akasema

“Kwa muda mrefu Marekani tumekuwa tunashirikiana na makundi kadhaa ya kigaidi katika mipango mbali mbali yenye maslahi kwa Marekani.Tumefanya hivyo katika nchi mbali mbali kama

vile..” Mark akanyamaza baada ya Rais William kuhamaki

“Kushirikiana na makundi ya kigaidi?akauliza William kwa mshangao

“Ndiyo mheshimiwa Rais” akajibu Mark

“Marekani haiwezi kushirikiana na magaidi hata siku moja.Tumekuwa vinara katika kupiga vita ugaidi duniani.Ni kwa juhudi hizo za kupamba na ugaidi tulifanikiwa kumuua Osama bin Laden kiongozi mkuu wa Alqaeda kundi la kigaidi lililokuwa hatari

duniani.Tumeendelea pia kuvisambaratisha vikundi mbali mbali vya kigaidi sehemu mbali mbali duniani.Nashangaa unaponiambia kwamba Marekani tunashirikiana na magaidi !

“Mheshimiwa Rais, ni kweli tunashirikiana na makundi ya kigaidi lakini hili ni suala la ndani mno na la siri kubwa.Hata marais waliopo madarakani huwa hawafahamishwi jambo hili na hawapaswi kulifahamu.Kwa ufupi tu ni kwamba kuna

kitengo maalum cha siri ndani ya CIA ambacho kinashughulikia mahusiano na mashirikiano na makundi ya kigaidi kwa maslahi ya Marekani.Kwa muda mrefu sasa Marekani tumekuwa tukivifadhili kwa pesa na silaha vikundi mbali mbali vya kigaidi ambavyo vimekuwa vikitekeleza mashambulio ya kigaidi sehemu mbali mbali duniani kwa maslahi ya Marekani”

“Mungu wangu ! akasema William akimtazama Mark Piller kwa macho ya woga

“Mheshimiwa Rais kama nilivyokueleza kwamba jambo hili ni la siri kubwa.Labda kwa kukupa mfano ni kwamba tumekuwa tukifadhili operesheni mbali mbali za kundi la kigaidi la IS sehemu mbali mbali duniani na moja kati ya operesheni ambazo tumetumia kundi la IS ni katika machafuko yanayoendelea Afrika Mashariki hivi sasa” akasema Mark na Rais William akasimama

“Machafuko ya Afrika mashariki yameratibiwa na

Marekani kwa kuwatumia IS?!
Rais William akashangaa

“Ndiyo mheshimiwa Rais.Ni mipango ya Marekani” akasema Mark na Rais William akasimama akamtazama Mark kwa mshangao mkubwa

“Mark naomba uniambie hiki unachonieleza si cha kweli” akasema William

“Mheshimiwa Rais ninachokueleza ni ukweli mtupu na jambo hili lina maslahi makubwa kwa Marekani” akasema Mark

“Mark watu wanakufa kama kuku Afrika Mashariki

hadi tumelazimika kutuma vikosi vyetu kwenda kusaidia kurejesha amani.Dunia inashuhudia machafuko makubwa kabisa ya kidini kuwahi kutokea halafu unaniambia kwamba ni kwa maslahi ya Marekan……”

“Mheshimiwa Rais ! akasema Mark na kumkatisha Rais William.

“Kinachoendelea hivi sasa Afrika Mashariki kina maslahi makubwa kwa Marekani.Tazama bei ya mafuta ilivyopanda katika soko la dunia baada ya nchi

wazalishaji wa mafuta kuweka mgomo baridi na kuzalisha kiwango kidogo cha mafuta kuliko mahitaji ya dunia.Hii imepelekea akiba yetu ya mafuta kuanza kupungua na wakati huo huo tuna migogoro na nchi nyingi ambazo ni wazalishaji wakubwa wa mafuta duniani.Hatuna mahusiano mazuri na Venezuela,Mashirikiano yetu na Saudi Arabia yametetereka pia,Iran ambao nao ni wazalishaji wakubwa wa mafuta ni maadui zetu,Iraq pia hatupati mafuta ya kutosha

kwani serikali iliyoko madarakani hivi sasa haitaki mashirikiano na Marekani.Nchi nyingine kama Urusi ambayo unafahamu mahusiano yetu nao.Nchi kamaLibya ambao wanashika nafasi ya tisa kwa akiba kubwa ya mafuta nako kumechafuka.Kwa ujumla mahusiano yetu na nchi wazalishaji wa mafuta duniani si mazuri na mafuta yetu hapa nchini hayatutoshi hivyo kwa namna yoyote ile tunahitaji kuongeza akiba yetu ya mafuta na Afrika Mashariki kuna kiasi

kikubwa cha mafuta.Nchi ya Uganda inakadiriwa kuwa na mafuta mengi zaidi kuliko nchi zote katika bara la Afrika hivyo mipango yetu kuhakikisha tunapata mafuta kutoka Uganda” akasema Mark Piller

“Mafuta? ! akauliza William kwa hasira

“Mafuta yana thamani kuliko uhai wa watu ? Sikutegemea kabisa kama Mark unaweza ukashiriki katika jambo hili ovu ! akasikitika Rais William

“Mheshimiwa Rais mafuta ni uchumi.Kuna mgomo baridi

kwa wazalishaji wa mafuta duniani.Hizi ni njama za wapinzani wetu dhidi ya uchumi wetu.Lazima tutumie kila njia kupata mafuta ndiyo maana tumeyafuata Afrika Mashariki.Mheshimiwa Rais yawezekana haya tunayoyafanya yasionekana sawa lakini ni kwa ajili ya nchi yetu.Marekani lazima iendelee kuwa taifa kubwa lenye uchumi mkubwa kuzidi yote duniani hivyo kila aina ya mbinu lazima itumike katika kuhakikisha hilo linatimia" akasema Mark

“Siamini kama ni wewe kweli Mark unayezungumza haya” akasema Rais William

“Mheshimiwa Rais,haya yote yanafanyika kwa maslahi ya Marek…….”

“Hata kama ni kwa maslahi ya Marekani hatukupaswa kusababisha machafuko yale yanayoendelea Afrika mashariki.Ule ni unyama uliovuka mipaka ya ubinadamu.Maiti za watu zimesambaa mitaani huku sisi tukifaidika kwa mafuta ambayo Mungu amewajalia wenzetu.Hili haliwezekani na

siwezi kulifumbia macho.Lazima nichukue hatua kalisana kwako na kwa wenzako wote mlioshirikiana kuandaa unyama wa namna hii Afrika Mashariki na kwingineko duniani ambako mmekwisha fanya !! akafoka William

“Mheshimiwa Rais usithubutu kufanya chochote kuhusiana na jambo hili.Hukupaswa kulifahamu suala hili lakini kwa kuwa u mtu wangu wa karibu nimeamua kukueleza kile kinachoendelea lakini kwa

kwaida Rais hapaswi kabisa kufahamu chochote kuhusiana na mambo haya nyeti mno kwa nchi” akasema Mark

“Mark huwezi ukanipangia nini cha kufanya.Mimi ni Rais wa Marekani na nitafanya kila niwezalo kuhakikisha ninakisambaratisha kikundi hicho cha wauaji ndani ya CIA.Siwezi kukubali wakaendelea na haya wanayoyafanya !

“Mheshimiwa Rais narudia tena kukuonya usithubutu kufanya chochote.Utaendelea kuufunga

mdomo wako kama vile hufahamu chochote kinachoendelea !

“Mtanifanya nini wewe na wenzako? Akauliza Rais William

“Utauawa ! akasema Mark na ukimya ukapita.William Washington alionyesha woga kwa kauli ile ya makamu wake Mark Piller

“Mheshimiwa Rais nakushauri fuata kile ninachokuelekeza.Ukienda kinyume chake basi sote maisha yetu yatakuwa hatarini”

“Kwa nini umenieleza jambo hili Mark wakati ukifahamu kuwa sipaswi kujua chochote? Akauliza Rais William

“Ni kwa sababu kuna mpango mkubwa unaoendelea kuhusu Iran ambao nataka uufahamu ili usiendelee na mipango yako ya kuivamia kijeshi Iran hadi mpango huo utakapokuwa umekamilika”

“Mpango gani Mark?akauliza Rais William akionekana kuanza kupunguza hasira alizokuwa nazo

“Nitakurejesha kwanza Afrika Mashariki.Mapinduzi yale yaliyofanywa na jeshi la Uganda yaliyomuondoa madarakani Rais Jenerali Akiki Rwamirama tuliyapanga sisi tukishirikiana na Rais wa Tanzania”

“Tanzania pia walishiriki katika mapinduzi yale?! Akauliza Rais William

“Kutokana na mashirikiano yetu na IS tuliweza kupata taarifa kuhusiana na mpango ulioshindwa kufanikiwa wa kuwaua marais wa Tanzania

na jamhuri ya kidemokrasia ya Congo kwa bomu la kujitoa muhanga.Katika mpango huo Jenerali Akiki pia alishiriki.Baada ya kupata taarifa hizo nilimtuma mjumbe maalum kwa Rais wa Tanzania akazungumza naye kuhusu kumuondoa madarakani Rais Akiki kwani tuliamini lazima atakuwa na hasira naye na ndipo ukaandaliwa mpango wa mapinduzi" akasema Mark

"Rais wa Tanzania naye alikubali yatokee haya yanaoendelea katika nchi

yake? Ni rais wa namna gani huyu ambaye anakubali kuona raia wake wakiuana namna ile? Akauliza Rais William kwa ukali

“Mpango wetu na Tanzania ulikuwa ni kumuondoa Jenerali Akiki madarakani na kuuweka utawala mpya.Baada ya mpango huo kukamilika ndipo tuliandaa haya machafuko yanayoendelea hivi sasa.Tulipanga kuanzisha vurugu nchini Uganda ili kuilazimisha serikali mpya ya kijeshi kutumia nguvu kubwa

kuzima vurugu hizo na kusababisha umwagikaji mkubwa wa damu hali ambayo ingepelekea kujengwa kwa chuki kubwa kati ya serikali na wananchi.Vurugu hizo zingekuwa kubwa na hivyo kuilazimisha Marekani kupeleka vikosi vyake Uganda na hapo ndipo tungepata nafasi ya kudhibiti visima vya mafuta na kuchukua kiasi cha mafuta tunachokihitaji.Ili kulifanikisha hilo tulihitaji msaada wa Jenerali Akiki.Haikuwa rahis kumfanya jenerali Akiki akubali

kushirikiana nasi hadi tulipotengeneza ajali ambayo iliripotiwa kwamba familia nzima ya Jenerali Akiki waliokuwa wanaelekea Dar es salaam walikoomba hifadhi baada ya kupinduliwa na jeshi walifariki”

“Subiri kidogo Mark.Umesema mlitengeneza ajali ambayo ilisadikisha watu kuwa familia yote ya Akiki walifariki katika ajali hiyo.Nini unakimaanisha? akauliza William

“Mheshimiwa Rais,familia ya Jenerali Akiki iko salama na

hawakufariki katika ile ajali kama ilivyodaiwa.Ajali ile ulikuwa ni mchezo ili kumpa hasira jenerali Akiki na kumfanya akubaliane na mpango wetu kwa nia ya kulipiza kisasi kwa wale walioua familia yake" akasema Mark Piller na Willim akaendelea kumtazama kwa macho ya mshangao

"Mark siamini kama haya maneno yanatoka katika kinywa chako.Iko wapi familia ya Akiki hivi sasa? Miili ile iliyosafirishwa katika majeneza kwenda Uganda ni

miili ya nani? Akauliza Rais William

“Mheshimiwa Rais familia ya Akiki kwa sasa iko sehemu salama katika nchi Fulani wakiishi kwa amani wakiwa chini ya uangalizi wa CIA.Wako salama kabisa wanatunzwa vizuri na wanapata kila wanachokihitaji.Katika yale masanduku kulikuwa na miili lakini haikuwa ya familia ya Akiki.Mheshimiwa Rais jambo hili limefanywa kitaalamu sana kiasi cha kutoweza kufahamika hadi leo hii ninapokueleza”

“Dah ! akasema Rais William halafu akainamisha kichwa akafikiri kwa muda kisha akamtazama Mark Piller na kusema

“Mark ninajaribu kuiaminisha akili yangu kwamba ni wewe ninaye kufahamu ndiye unanieleza haya au ni Mark mwingine”

“Ni mimi mheshimiwa Rais.Najua haya niliyokueleza yamekustua sana lakini naomba usistuke kwani yote ni mipango kwa ajili ya nchi yetu” akasema Mark na kunyamaza kidogo

“Baada ya kumleta Akiki hapa Marekani nilizungumza naye akakubali kushirikiana nasi kuanzisha vurugu Uganda na akashauri njia pekee ya kuweza kuleta machafuko nchini Uganda ni kwa kutumia dini.Alishauri kama tukiweza kuwafarakanisha waumini wa dini ya kikristu na kiislamu lazima machafuko makubwa yatatokea.Akiki alikwenda mbali zaidi akashauri kwamba kama tunataka kuchukua mafuta basi machafuko ya Uganda pekee hayataweza kutusaidia bali tunahitaji

kueneza machafuko hayo hadi nchini Tanzania kwani bomba la mafuta linatoka Uganda hadi Tanga nchini Tanzania ambako ndiko meli zetu zingeweza kupakia mafuta.Tuliuchukua ushauri huo na kuanzia hapo tuliwahitaji IS ili waweze kuanzisha choko choko za kidini nchini Uganda na Tanzania.Vile vile kwa msaada wa Akiki tuliweza kuwapata mwanasiasa mmoja wa Uganda na mwingine wa Tanzania ambao wangeweza kuchochea vurugu hizo katika

nchi zao na wanasiasa hao pamoja na wale viongozi wa dini kwa sasa wako hapa Marekani.Tulikubaliana baada ya vurugu hizo kuanza watakuwa wameimaliza kazi yao na watakuja kuishi Marekani.IS walifanya mauaji ya viongozi wa dini na kusababisha hasira na chuki kubwa miongoni mwa waumini wa dini hizo na Yule mwanasiasa wa Uganda akawachochea viongozi wa dini ya kikristu kuanzisha mashambulizi dhidi ya nyumba za ibada za waislamu

na hapo ndipo machafuko yalipoanzia.Vurugu zilipoenea Uganda tulihamia pia Tanga Tanzania ambako nako vurugu zikaenea na kusambaa katika sehemu mbali mbali za Tanzania.Mheshimiwa Rais hivyo ndivyo ilivyokuwa hadi tukafanikiwa kupeleka vikosi vyetu Afrika Mashariki na sasa meli zetu zimepanga foleni katika bandari ya Tanga nchini Tanzania zinapakia mafuta na hifadhi yetu ya mafuta inaongezeka.Hatuna tena sababu ya kusumbuka na mafuta ya kutoka Mashariki ya

kati.Hadi vurug hizi zitakjapomalizika tutakuwa na akiba kubwa sana ya mafuta.Pima mwenyewe mheshimiwa Rais je hiki kilichofanyika kina maslahi kwa nchi yetu au hakina? Akauliza Mark Piller na Rais Wiliam akavuta pumzi ndefu

“Mark mlichokifanya kweli kina maslahi makubwa kwa nchi yetu kwani tunahitaji sana mafuta lakini tatizo ni njia mliyotumia.Tumemwaga damu za watu kwa ajili ya kujipatia mafuta.Machoni pa

Mungu hii si sawa hata kidogo” akasema William

“Nakubali mheshimiwa Rais lakini tumekuwa tukifanya hivi kila mara na hakukuwa na namna nyingine ya kufanya kuweza kujipatia mafuta zaidi ya kutumia njia hii” akasema Mark Piller

“Kwa nini mkaniweka kando kuhusiana na masuala haya?Kama si wewe kuamua kunieleza leo hii nisingefahamu chochote kuhusu kile kinachoendelea.Niliposhauriwa tupeleke vikosi vyetu Afrika

mashariki niliamini ni kwa nia njema ya kuzuia mauji kuendelea kumbe ni mpango umetengenzwa ili tukachukue mafuta”

“Mheshimiwa Rais kama nilivyokueleza awali kwamba mambo haya yanafanywa kwa siri kubwa sana na Rais wa nchi hatakiwi kabisa kufahamu kitu chochote na hata mimi kukueleza nimevunja kanuni zetu kwani iwapo nitagundulika nitauawa hivyo ni jukumu lako kuufunga mdomo wako ili mimi na wewe tuendelee kuwa salama”

akasema Mark Piller na ukimya ukatawala.

“Mheshimiwa Rais ! akasema Mark Piller na Rais William aliyekuwa ameinamisha kichwa akainua kichwa akamtazama

“Katika mpango huu unaoendelea Afrika Mashariki kuna mpango mwingine umezaliwa ndani yake ambao nao una manufaa makubwa sana ambao unahusiana na Iran”

“Una mpango gani kuhusu Iran?akauliza William

“Nilikueleza awali kwamba kwa muda mrefu tumekuwa tukiichunguza Iran kufahamu silaha zake bila mafanikio.Nimekuja na mpango mpya ambao unaweza ukatusaidia kufahamu kuhusu silaha za Iran na vile vile kulipua kinu kikubwa ambacho Iran inakitegemea katika kurutubisha madini ya Urani” akasema Mark Piller na ile mikunjo katika sura ya Rais William Washington ikatoweka

“Nieleze kuhusu mpango huo.Nini umekibuni? Akauliza Rais William

“Kuna mtu ambaye tumekuwa tukimtumia katika mipango yote ya kufadhili vikundi vya kigaidi ambavyo tuna mashirikiano navyo.Mtu huyo ni mwanamama anaitwa Habiba Jawad.Huyu ni raia wa Saudi Arabia.Mume wake ndiye tuliyekuwa tukimtumia katika kazi hiyo lakini baadae alionyesha mabadiliko na tukalazimika kumuua.Baada ya kuuawa mkewe akarithi utajiri wote na akaendelea

kuifanya ile kazi aliyokuwa anaifanya mumewe yaani kufadhili makundi ya kigaidi.Tulimuwezesha kimtaji na utajiri wake ni mkubwa sana.Ni mmoja kati ya mabilionea wa Saudi Arabia na mwanamama mwenye heshima kubwa.Toka alipochukua jukumu hili amelifanya kwa ufanisi mkubwa.Mpaka sasa yeye ndiye anayetambulika kama mfadhili mkuu wa kundi la IS na makundi mengine madogo madogo ya kipalestina yanayopigana na serikali ya

Israel.Ni kwa sababu yake hadi leo dunia haifahamu kama Marekani ndio wafadhili wakuu wa kundi la IS na itabaki hivyo.Hata ndani ya IS ni watu wachache tu wanaolifahamu hilo”

“Sifahamu hayo yote unayonieleza Mark”akasema Rais William

“Hupaswi kuyafahamu mheshimiwa Rais.Si wewe tu bali rais yeyote wa Marekani hapaswi kuyafahamu haya”akasema Mark Piller

“Mheshimiwa Rais,Habiba Jawad anakuja

Marekani.Ananiletea mtu mmoja ambaye amekubuhu katika masuala ya ugaidi.Mtu huyo tutamtuma Iran”

“Sijakuelewa Mark.Tutamtumaje gaidi kwenda Iran?Tunamtuma akafanye nini?

“Gaidi huyo ambaye Habiba anakuja naye ndiye atakayekwenda Iran kuchunguza kuhusu silaha za Iran na mfumo wake wa makombora na vile vile kuharibu kinu kikubwa ambacho Iran inakitegemea katika urutubishaji wa madini

ya Urani” akasema Mark na Rais William akajikuta akitoa kicheko

“Sikupaswa kucheka lakini Mark umenifanya nicheke.Kwa nini umtume gaidi Iran badala ya majasusi wetu? Magaidi hawana mafunzo yoyote wao wanachofahamu ni kuua tu.Mpango huo ni wa chini sana kufanywa na taifa kubwa kama la Marekani lenye maelfu ya majasusi wenye ujuzi wa hali ya juu mno.Tuna shirika kubwa la ujasusi kuliko yote duniani.Tuwatumie hao kuliko kumtuma gaidi

akafanye kazi kwa niaba yetu.Huu ni mpango wa aibu” akasema Rais William

“Mheshimiwa Rais,nimekuwa ndani ya CIA kwa muda mrefu.Hakuna kitu ambacho kinaumiza vichwa vya watu wa CIA kama suala la Iran na Korea Kaskazini.Pamoja na kuwa na majasusi wa kiwango cha juu mno bado mpaka leo hatujafanikiwa kufahamu kuhusu mfumo wa makombora wa Iran au silaha inazomiliki.Na hili ndilo ambalo limeleta ugumu mpaka

leo tunasita kuitandika Iran kijeshi kwani hatuna uhakika yawezakana akawa kweli anamiliki silaha za maangamizi makubwa kama wanavyodai.Kwa kuwa majasusi wetu wameshindwa tunataka kujaribu njia ya pili ambayo ni kumtumia gaidi” akasema Mark Piller

“Hiki ni kichekesho Mark.Gaidi anawezaje akaingia Iran na kufanya uchunguzi kuhusu silaha zake?

“Mpango uko hivi mheshimiwa Rais” akasema

Mark Piller na kunyamaza akanywa maji kulainisha koo.

“Gaidi huyo tutampeleka Afrika Mashariki ambako atalipua ubalozi wetu jijini Dar es salaam”

“Kulipua ubalozi wa Marekani ?! William akahamaki

“Ndiyo mheshimiwa Rais”

“Hilo ni jambo lisilowezekana kabisa.Hatuwezi kumtuma mtu akalipue ubalozi wetu na kuua watu wetu ! akasema kwa ukali Rais William

“Tayari tumekwisha fanya hivyo jijini Kampala mheshimiwa Rais.Ubalozi wetu kule ulivamiwa na kuchmwa moto ule ulikuwa ni mpango maalum umepangwa ili kuwafanya wamarekani wakubaliane na hatua ya kupeleka vikosi vyetu Uganda” akasema Mark Piller

“Mungu wangu ! akasema William akimtazama Mark Piller kana kwamba ni mara ya kwanza anakutana naye

“Mheshimiwa Rais” akaendelea Mark

“Tutaulipua ubalozi wetu jijini Dar es salaam kisha tutamkamata huyo gaidi na kumpeleka mafichoni” akasema Mark na kunyamaza kidogo

“Miaka sita iliyopita ndege ya shirika la ndege la Qatar ikitokea Moscow Urusi kuelekea Tehran ikiwa na abiria mia moja ishirini na saba ndani yake ililazimika kutua kwa dharura katika uwanja wa ndege wa Almaty nchini Kazakhstan kufuatia hitilafu iliyojitokeza katika mojawapo ya injini zake.Baada

ya kutua abiria wote walishushwa ndegeni na kupelekwa hospitali kwa uchunguzi wa afya zao kufuatia wengi wa abiria kupatwa na mstuko mkubwa kutokana na tukio lile.Mheshimiwa Rais sisi ndio tuliotengeneza tukio lile hadi ndege ikatua nchini Kazakhstan.Tulikuwa na sababu maalum" akasema Mark na kunyamaza kidogo halafu akaendelea.

"Miongoni mwa abiria wa ndege ile,walikuwemo wanasayansi sita wa Iran wakitokea nchini Urusi

ambako walikwenda kupatiwa mafunzo ya siri namna ya kutengeneza bomu la nyuklia.Tulizipata taarifa hizo na kutengeneza mpango ule kisha tutakafanikiwa kuwapata wanasayansi hao ambao tunaendelea kuwashikilia hadi sasa tukiendelea kuwahoji japo hawajasema chochote”

“Wako wapi hao wanasayansi?

‘Tunaendelea kuwashikilia katika mojawapo ya nyumba salama za CIA” akajibu Mark

“Gaidi tunayekusudia kumtuma kulipua ubalozi wetu

Dar es salaam atakamatwa baada ya kutekeleza shambulio hilo.Kisha kamatwa atakwenda kuunganishwa na wanasayansi hao mahala walikofichwa na kujenga ukaribu nao.Baada ya kuzoeana nao atasuka mpango wa kuwatorosha wanasayansi hao na wakifanikiwa kutoroka wataelekea moja kwa moja nchini Iran.Serikali ya Iran itakuwa na kila sababu za kumuamini huyo gaidi kwani kwa wakati huo dunia nzima itakuwa ikifahamu kitu alichokifanya yaani kulipua ubalozi wa Marekani na Iran

watampokea kama shujaa.Akiingia Iran ndipo atakapoanza kuifanya kazi yetu tuliyomtuma” akasema Mark Piller na ukimya ukatawala mle ndani halafu Rais William akasema

“Mark huo unaonekana ni mpango mzuri sana lakini tatizo ni huyo jamaa ambaye unataka kumtumia katika mpango huo.Hana mafunzo ya kijasusi na hawezi kutekeleza vyema kazi aliyotumwa na nina wasi wasi anaweza akagundulika kuwa ametumwa na Marekani na akauawa hivyo

tukakosa kila kitu”Rais William akaonyesha wasiwasi mkubwa

“Hata kama akigundulika kwamba ametumwa na Marekani tutakana tuhuma hizo na dunia itatuelewa kwanza mtu huyo si raia wa Marekani na kwa wakati huo atakuwa anajulikana kama gaidi ambaye anatafutwa na Marekani kwa kulipua ubalozi wake jijini Dar es salaam na vile vile atakuwa anatafutwa kwa kutoroka kutoka katika mahala alipokuwa anashikiliwa.Kwa sababu hizo

mbili tutakuwa tumejitoa katika jambo hilo lakini kwa namna mpango ulivyo uhakika wa mtu huyo kugundulika ni mdogo sana”

“Yawezekana mkawa mmejipanga vizuri kabisa lakini tatizo ni uwezo wa huyo gaidi kutekeleza mpango mkubwa kama huu.Jambo kama hili linahitaji jasusi mbobezi.Tunao wengi sana majasusi wa namna hiyo ambao tunaweza kuwatumia katika mpango huo.Kwa nini tusitafute mmoja wao tukamtumia badala ya huyo

gaidi? Sijaukataa mpango huu lakini sikubaliani na mtu mnayetaka kumtumia.Ni mpango mzuri sana na kama ungeniambia kwamba anayekwenda kuutekeleza ni jasusi nguli wa Marekani basi ningekubaliana nawe kwa asilimia mia moja lakini kwa gaidi kwenda kutekeleza mpango huo nashindwa kukubaliana nawe Mark”

“Mheshimiwa Rais,hatutaki kumtumia raia wa Marekani katika jambo hili.Mtu huyo ambaye Habiba anakuja naye ni raia wa Saudi

Arabia ambao hawana maelewano mazuri na Iran.Endapo misheni itashindwa kufanikiwa na mtu huyo akakamatwa basi mzozo utakuwa ni kati ya Iran na Saudi Arabia sisi hatutahusika.Kwa mujibu wa Habiba Jawad mtu huyo anayemleta ni mtu mahiri na sahihi kwa kazi hiyo.Atakapokuja hapa tutampima na kuona uwezo wake lakini sina wasiwasi naye hata kidogo.Ninamuamini Habiba Jawad.Nina uhakika mkubwa mtu anayemleta

atakwenda kuitekeleza vyema kazi tutakayomtuma akaifanye Iran”

“Mark nina wasi wasi sana kuhusu jambo hili unalotaka kulifanya.Sijui kwa nini ninakuwa na wasiwasi mkubwa namna hii” akasema Rais William

“Naomba uniamini mheshimiwa Rais.Nina uhakika mkubwa sana na hiki ninachokwenda kukifanya.Tumekuwa tukifanya mambo kama haya sehemu mbali mbali na tukafanikiwa.Mheshimiwa

Rais katika haya yanayoendeleaAfrika Mashariki tutaua ndege wawili kwa jiwe moja.Tunaongeza akiba ya mafuta na vile vile kwa mara ya kwanza tutafanikiwa kujua aina ya silaha ilizo nazo Iran.Haya ni mafanikio makubwa sana mheshimiwa Rais" akasema Mark Piller

"Mark katika suala la mafuta japo mmetumia njia ambayo si ya kibinadamu lakini nataka niwapongeze.Tunahitaji sana mafuta na nchi za Mashariki

ya kati ambazo ni wazalishaji wakubwa wa mafuta duniani ziko katika mgomo baridi wa kuzalisha mafuta kwa lengo la kutukomoa sisi kutokana na sera zetu za kuiunga mkono Israel.Wamesahau kwamba Marekani wana uwezo wa kupata mafuta kutoka sehemu yoyote ile wanayoitaka.Kwa sasa mafuta kutoka Afrika yanaendelea kumiminika katika hifadhi zetu za mafuta.Hongereni sana Mark.Japo niliwekwa pembeni katika jambo hili lakini lazima niwapongeze.”

“Ahsante sana mheshimiwa Rais” akasema Mark Piller

“Kuna kitu nataka kukiongeza hapo.Eneo hili la ukanda wa Afrika Mashariki ni tajiri sana.Lina utajiri mkubwa wa madini mbali mbali ambayo tunayahitaji mno.Kwa mfano nchini Tanzania pekee yanapatikana madini ya thamani kubwa yanaitwa Tanzanite ambayo hayapatikani sehemu nyingine yoyote duniani zaidi ya Tanzania,yapo pia madini mengine kama

dhahabu,almasi,na zaidi sana madini ya Urani.Ukienda Uganda kuna mafuta,ukienda jamhuri ya kidemokrasia ya Congo kuna madini mengi pia ya thamani kubwa.Kwa ujumla eneo hili lote limejaa madini.Kwa kuwa tayari tumekwisha ingia Afrika Mashariki ni jukumu letu kuhakikisha tunajiimarisha na tunakwenda mbali zaidi ya mafuta.Wekeni mikakati ya kuhakikisha tunaongeza vikosi zaidi Afrika Mashariki na tunakwenda mbali zaidi kwa kupeleka vikosi vyetu sehemu

zile zenye utajiri lakini jambo hili lifanyike kwa ustadi na umakini mkubwa kama mlivyofanya katika haya machafuko.Nataka hadi tutakapoondoa vikosi vyetu Afrika mashariki tuwe tumefaidika na akiba kubwa ya mafuta na madini mengine ya thamani”akasema Rais William

“Mheshimiwa Rais ninashukuru kwa kuanza kuelewa kile tunachokifanya kwa ajili ya nchi yetu.Ili tuendelee kujiimarisha na kukaa muda mrefu zaidi Afrika

Mashariki inatulazimu kutafuta namna ya kuongeza machafuko katika ukanda huo wa Afrika Mashariki.Nitakaa na wenzagu tuone namna ya kufanya lakini kuna kitu ninakifikiria ambacho kinaweza kutupa sababu ya kuongeza vikosi vyetu na tukaendelea kuchota Rasilimali" akasema Mark Piller

"Nini unakifikiria kuhusiana na hilo wazo langu? Akauliza William

"Kutoka katika machafuko haya yanayoendelea Afrika

Mashariki ninafikiria kuanzisha kikundi cha uasi ambacho tutakipa nguvu na kukifadhili silaha kali ambacho kitasambaa katika nchi za Tanzania na Uganda.Hatuna shida sana na nchi ya Kenya.Shida yetu ni Tanzania,Uganda na jamhuri ya kidemokrasia ya Congo nchi ambazo zina utajiri mkubwa.Kikundi hicho ambacho kitasambaa katika nchi hizo tatu kitawezeshwa silaha nzito na kuendelea kulifanya eneo la Afrika mashari liwe ni eneo hatari na

sisi tutaongeza vikosi vyetu Afrika Mashariki kulinda amani.Nitazungumza na Jenerali Akiki kuhusiana na suala hili na tutaona nini tukifanye lakini nakuhakikishia mheshimiwa Rais kwamba haya maelekezo yako yatafanyiwa kazi.Ninachokuomba niamini na kila kinachoendelea nitakujulisha lakini nakuomba haya niliyokwambia iwe ni siri yako asifahamu mtu mwingine yeyote mambo haya.Narudia kukupa angalizo mheshimiwa Rais kwamba endapo haya

niliyokwambia yatavuja utakuwa ni mwisho wetu.Hii ni moja kati ya siri kubwa sana ya nchi ya Marekani” akasema Mark Piller

Mazungumzo yao yalidumu kwa saa tatu kisha wakaagana na Mark Piller akaondoka zake.

DAR ES SALAAM – TANZANIA

MAKAO MAKUU YA SNSA

Saa mbili za asubuhi wafanyakazi wa idara ya siri ya usalama wa ndani wa nchi wakiwa katika ofisi yao kuu wakiendelea na majukumu yao katika ukumbi mkubwa waliyaelekeza macho yao katika runinga kubwa mbili wakifuatilia picha kutoka katika drone kubwa zilizokuwa zinazunguka angani juu ya jiji la Dar es salaam kufuatilia hali inavyokwenda.Mitaa mingi

hata ile ambayo ilizoeleka kuwa na msongamano mkubwa wa watu ilikuwa mitupu.Makundi ya watu yakijiandaa kwa ajili ya kuendelea na mapambano yalionekana katika sehemu mbali mbali za jiji.Vikosi vya ulinzi viliendelea kufanya doria katika baadhi ya mitaa lakini barabara nyingi zilikuwa zimefungwa kwa kuwekwa mawe makubwa na kuchomwa matairi.Katika baadhi ya picha yalionekana majengo yakiungua moto.Maiti za watu

zilionekana pia katika baadhi ya mitaa.

Wakati wafanyakazi wale wakiendelea kufuatilia picha zile,katibu muhtasi wa Ruby akamfuata na kumjulisha kwamba Rais anataka kuzungumza naye katika simu.Haraka haraka Ruby akaenda ofisini kwake na kuinua mkono wa simu

“Mheshimiwa Rais shikamoo” akasema Ruby

“Marahaba Ruby vipi mnaendeleaje?akauliza Rais Dr Fabian

“Tunaendelea vizuri mheshimiwa Rais.Tunafuatilia picha za drone kuona namna hali ilivyo katika mitaa mbali mbai ya jiji lakini hali bado ni tete.Barabara nyingi zimefungwa,majengo yanaungua moto makundi ya watu wanaendelea kujiandaa kuingia mitaani katika vurugu.Huduma hazipatikani na maisha yanazidi kuwa magumu” akasema Ruby

“Nimepokea taarifa asubuhi hii kutoka kwa mkuu wa jeshi la polisi kwamba bado hali ni tete huko mitaani.Hata

hivyo nimekupigia kukujulisha kwamba ndani ya dakika kumi zijazo mawasiliano ya simu yatarejeshwa kama ulivyokuwa umeshauri na baadae nitalihutubia taifa ili tuone kama inaweza ikasaidia kupunguza vurugu hata kwa kiasi kidogo” akasema Dr Fabian

“Ahsante sana mheshimiwa rais kwa kulifanya kazi suala hili.Nina uhakika linaweza kuwa na matokeo mazuri na watu wakakuelewa” akasema Ruby

“Ruby kubwa ambalo limenifanya nitake mawasiliano ya simu yarejeshwe ni ili kuwawezesha kumfuatilia Karim.Mliniambia kwamba kukosekana kwa mawasiliano kumewafanya mkashindwa kumfuatilia Yule jamaa.Mawasiliano yatarejea muda si mrefu nataka mumfuatilie Karimu na kuhakikisha mnafahamu kila kitu kuhusu yeye na jioni ya leo nipewe taarifa kama tayari mmemkamata au vipi” akasema Dr Fabian

“Mheshimwia Rais tutalifanyia kazi suala hilo na jioni ya leo nitakujulisha kile ambacho tutakuwa tumekipata katika uchunguzi wetu kuhusiana na Karim Abdallah” akasema Ruby na kuagana na Rais kisha akakaa katika kompyuta yake kwa dakika tano akafanya kazi fulani halafu akarejea katika ule ukumbi mkubwa ambako wafanyakazi wa SNSA walikuwa wanaendelea kufuatilia picha za Drone kujua hali ilivyo katika mitaa

mbali mbali ya jiji la Dar es salaam.

“Naomba tusikilizane jamani” akasema Ruby na watu wote wakawa makini kumsikiliza

“Toka machafuko haya yalipoanza mawasiliano ya simu yalikatwa kwa lengo la kuzuia watu kutumia simu kuhamasishana kuhusu vurugu.Pamoja na kukata mawasiliano ya simu lakini bado haijasaidia kupunguza vurugu” akanyamaza kidogo halafu akaendelea

“Muda mfupi uliopita nimetoka kuzungumza na mheshimiwa Rais na amenieleza kwamba ndani ya dakika chache zijazo mawasiliano ya simu yatarejeshwa” akanyamaza baada ya watu kushangilia

“Jana usiku tulikuwa na mazungumzo na Rais tukamuomba aruhusu mawasiliano ya simu yarejeshwe na amekubali ombi letu hivyo ndani ya muda mfupi mawasiliano ya simu yatarejea.Kubwa ambalo lilinifanya nimuombe Rais

aruhusu mawasiliano ni kwa ajili ya kumchunguza huyu mtu” akasema Ruby na kubonyeza kitanza mbali na picha ya Karim Abdallah ikaonekana runingani

“Anaitwa Karim Abdallah.Ni mwenyekiti wa chama cha siasa cha TPD.Kwa nini ameonekana katika runinga yetu? Huyu jamaa kabla machafuko hayajaanza aliandika ujumbe wa uchochezi katika ukurasa wake wa twitter akiwataka waislamu wa mkoa wa Tanga waungane wakawatafute wale waliomuua

Sheikh mkuu wa mkoa huo aliyeuawa na watu wasiojulikana.Ujumbe huo japo aliufuta haraka lakini tayari ulikwisha somwa na watu wengi.Tunajiuliza nini sababu ya kuandika ujumbe kama ule? Kuna wasiwasi machafuko haya yanayoendelea yakawa na chembe chembe za kisiasa ndani yake hivyo nataka mawasiliano yatakaporejea tuanze kumfukua huyu jamaa kufahamu kila taarifa zake.Tunahitaji kujua mahala alipo,kufahamu nani

anawasiliana nao na wanawasiliana nini,marafiki zake ni akina nani.Kwa ujumla nataka tufahamu kila kitu kumuhusu huyu jamaa.Sasa kila mmoja aende mahala pake na tuanze kazi mara moja” akasema Ruby kisha akaelekea ofisini kwake akaichukua simu yake akaiwasha tayari mawasiliano yalikwisha rejea.

“Ahsante Mungu.Sasa kazi inaanza”akasema Ruby

RIYADH – SAUDI ARABIA

Toka Mathew alipoondoka na Habiba kuelekea Marekani,Najma hakutoka ndani.Alikuwa amejifungia chumbani kwake akiwa na mawazo mengi sana.Pembeni yake kulikuwa na simu ya Mathew pamoja na kitabu cheusi.Aliishika simu ile na kuitazama halafu akairusha pembeni

“Huyu Ruby ambaye Abu ameandika namba zake za simu katika kitabu chake cha kumbu kumbu ni nani?Kwa nini nilipomuuliza Ruby ni

nani alibadilika na haraka haraka akaninyang'anya kile kitabu? Akawaza Najma.

"Katika simu yake amepiga namba za Ruby zaidi ya mara tatu lakini kwa bahati mbaya simu hiyo haikuwa ikipatikana.Tatizo langu nina wivu mbaya mno na hii ndiyo sababu kubwa iliyonifanya nikawa sitaki kuingia katika masuala ya mahusiano.Ninampenda sana Abu Zalawi na sitaki awe na mwanamke mwingine zaidi yangu" akaendelea kuwaza Najma

“Najilaumu sana kwa kuingia katika mahusiano na Abu Zalawi bila kuifahamu historia yake ametoka wapi na maisha yake yalikuwaje huko alikotoka.Je alikuwa na mke au na familia?Hata yeye mwenyewe hajawahi kunieleza chochote kuhusiana na historia yake” Najma akainuka kitandani na kukaa

“Lakini kwa nini niteseke wakati namba za simu za huyo Ruby ninazo? Kwa nini nisimpigie kuufahamu ukweli?Yawezekana akawa ni rafiki yake au ni mtu ambaye

waliwahi kuifanya kazi wote.Nimepata wivu kwa sababu Abu hajawahi kuonyesha kumafuta simuni mwanamke kama alivyofanya kwa Ruby jana” Najma akaendelea kutafakari

“Hapana siwezi kuendelea kuumia.Ngoja nimpigie simu huyu Ruby nimfahamu vizuri na nifahamu ana mahusiano gani na Abu” akawaza Najma na kubonyeza namba zile za Ruby akapiga simu ikaanza kuita akahisi kama mwili unamtetemeka.

“Simu yake inaita” akawaza huku akihisi woga kwa mbali

“Hallow ! ikasema sauti ya mwanamke upande wa pili wa simu na Najma akasita kujibu

“Hallow ! ikaita tena sauti ile

“Hallow ! akasema Najma kwa lugha ya kiingereza

“Habari yako?akauliza Yule mwanamke upande wa pili

“Nzuri habari yako?

“Nzuri.Nazungumza na nani kutokea wapi?

“Naitwa Najma niko Riyadh Saudi Arabia”

“Riyadh ! Yule mwanamke akaonyesha mshangao

“Ndiyo.Wewe uko wapi?akauliza Najma na Yule mwanamke akasita kidogo

“Hallow ! Najma akaita

“Najma umenifahamuje?Umepata wapi namba zangu za simu?

“Unamfahamu Abu Zalawi? Akauliza Najma

“Abu Zalawi?yule mwanamke akashangaa

“Ndiyo unamfahamu? Najma akauliza

“Hapana simfahamu.Ni nani huyo mtu?

“Ni mume wangu lakini ana namba zako katika kitabu chake cha kumbukumbu za mawasiliano na jana alikupigia simu mara tatu lakini simu yako haikuwa ikipatikana” akasema Najma

“Utanisamehe dada yangu lakini simfahamu mtu mwenye jina hilo na wala sijawahi kuwa na rafiki mwenye jina hilo la Abu Zalawi.Ni mara ya kwanza ninalisikia”

“Abu ameandika namba zako za simu katika kitabu

chake na alikupigia alionekana ana jambo la muhimu sana anataka kukueleza.Kwani wewe si Ruby?akauliza Najma na mwanamke wa upande wa pili akasita

“Hallow? Najma akaita

“Nakuuliza kwani wewe si Ruby?Najma akauliza tena

“Naweza kuzungumza na huyo Abu Zalawi ” akauliza Yule mwanamke

“Abu Zalawi amesafiri Alfajiri ya leo.Naomba tafadhali kama akikupigia tena simu usimwambie chochote kuhusu mimi kukupigia

simu.Ahsante sana nimefurahi kuzungumza nawe japo umekataa kunitajia jina lako” akasema Najma na kukata simu akashusha pumzi na kutazama namba zile halafu akaigiza namba za mwanzo katika kompyuta yake ili kujua namba zile ni za nchi gani na majibu yakaja kuwa ni Tanzania.

“Tanzania ! akasema Najma na kuvuta pumzi ndefu

“Niliona kwa macho yangu mawili katika kitabu chake ameandika jina Ruby.Iweje huyu mwanamke niliyempigia

ambaye japo amekataa kunitajia jina lake lakini naamini ni Ruby akane kumfahamu Abu? Akajiuliza Najma

“Au Abu ana jina lingine anatumia tofauti na Abu Zalawi?Amefahamiana vipi na uyu mwanamke wa Tanzania?” akawaza Najma

“Ninahitaji kumfahamu Abu Zalawi kiundani na mtu pekee ambaye anaweza akanieleza kila kitu kuhusiana na huyu mtu ni mama.Atakaporejea katika hiyo safari waliyokwenda

nitamtaka anieleze ukweli kuhusiana na Abu Zalawi kwani kuna mambo yameanza kunipa mashaka sana kuhusiana na huyu mtu.Mama amefahamiana vipi na Abu?Kuna kitu gani wanakipanga? Nitafahamu kila kitu watakaporejea” akawaza Najma

DAR ES SALAAM – TANZANIA

Ruby aliendelea kuishikilia simu yake baada ya kuzungumza na Najma.

“Abu Zalawi ! akajiuliza

“Ni nani huyo mtu? Sijawahi kuwa na rafiki yeyote mwenye jina hilo la Abu Zalawi wala sina rafiki yeyote Saudi Arabia sasa huyu mtu amenifahamuje hadi ana namba zangu tena ninazotumia hapa Tanzania ? Sijawahi kumpa namba za simu ninazotumia Tanzania mtu wangu yeyote wa nje ya

nchi,huyu Abu Zalawi amezpata wapi?” akajiuliza Ruby

“Au labda Uingereza wamekwisha gundua kwamba sikufariki katika ile ajali ya ndege na sasa wanaanza kunichunguza ili wapate uhakika kama ni mimi? Akaendelea kujiuliza

“Kwa nini nisimpigie simu Najma na kumtaka anitumie picha ya huyo Abu Zalawi nimuone kama ninamfahamu? Nadhani hilo litakuwa jambo jema” akawaza na kuchukua simu akampigia Najma kwa

kutumia zile namba alizompigia.

“Hallow” akasema Najma baada ya kupokea

“Najma samahani sana kwa usumbufu,Unaweza ukanitumia picha ya Abu Zalawi nimuone kama ni mtu ninayemfahamu?akauliza Ruby

“Sawa ninakutumia muda si mrefu” akasema Najma na kupekua simu ya Mathew lakini hakukuwa na picha hata moja ya Mathew.Akapekua katika simu yake lakini

hakukuwa na hata picha moja ya Mathew akachanganyikiwa

“Haya mbona ni maajabu makubwa.Picha zote zimekwenda wapi? Tumepiga picha nyingi sana tukiwa katika mapumziko.Ni maelfu ya picha lakini hakuna hata picha moja na sielewi zimekwenda wapi” akawaza na kuchukua kamera yake ambayo nayo pia alikuwa anaitumia wakati wakiwa mapumzikoni lakini hakukuwa na picha hata moja.

“Mungu wangu haya mbona maajabu? Akasema

kwa mshangao na kuchukua kompyuta yake mpakato na haraka haraka akafungua sehemu ya kuhifadhi picha ambako alikuwa anahifadhi picha kila pale kadi ya kuhifadhia kumbu kumbu ilipojaa lakini akakutana na kioja kwani zile picha zote ambazo walipiga katika mapumziko hazikuwepo.

“Jamani haya ni mambo gani yanatokea?Tumepiga maelfu ya picha kwa miezi mitatu na hata jana nilikuwa nazitazama nikichagua zile nzuri kwa ajili ya kuweka

kumbu kumbu lakini ajabu leo hii hakuna hata picha moja.Hakuna picha katika simu yangu,ya Abu,katika kamera na hata katika kompyuta.Zimekwenda wapi?Nani amezifuta na kwa nini?akajiuliza na mara simu yake ikaita tena akazitazama zile namba ni Yule mwanadada aliyempigia kutoka Tanzania

“Nitamjibuje huyu dada? Ataniona mwongo” akawaza Najma halafu akaipokea ile simu

“Najma samahani umeipata picha hiyo ya Abu Zalawi?akauliza

“Hapana bado.Nitakutumia baadae kidogo naomba unisubiri” akasema Najma na kukata simu.

“Haya ni maajabu ambayo sijawahi kuyashuhudia” akawaza na kuendelea kupekua kompyuta yake kama angeweza kupata picha zile akini hakukuwa na picha yoyote

“Humu ndani hakuna mtu mwingine yeyote aliyeingia

zaidi yetu mimi na Abu.Kama angekuwa mtu mwingine ameingia ningehisi labda ndiye aliyefuta picha hizo lakini hakuna tulikuwa humu watu wawili pekee.Ningeweza kusema ni kirusi labda kimefuta picha hizo lakini picha zilizofutwa ni zile nilizopiga na Abu pekee nyingine zote zipo" akawaza na kushika kidevuni

"Hapa kuna kitu kinaendelea.Picha zile hazijajifuta zenyewe bali zimefutwa kwa sababu maalum na aliyezifuta lazima

atakuwa ni Abu.Kwa nini akafanya hivi? Amefuta muda gani hizo picha? Najma akapandwa na hasira

“Huyu Abu Zalawi ni nani hasa?Mbona anaanza kunipa mashaka? Nadhani nahitaji kumfahamu kwa undani zaidi ni mtu wa aina gani huyu.Yawezekana ninavyomfahamu sivyo alivyo” akaendelea kuwaza Najma.

****

Ruby alitoka ofisini kwake akamfuata Gosu Gosu

“Nikiiona tu sura yako ikiwa namna hiyo najua kuna kitu hakiko sawa.Kuna habari mbaya?Gosu Gosu akauliza mara tu Ruby alipoingia ofisini kwake

“Gosu Gosu kuna kitu kimetokea kinanipa wasi wasi kidogo” akasema

“Nini kimetokea Ruby?Nieleze tafadhali”

“Nimepigiwa simu muda mfupi uliopita na mwanamke mmoja anaitwa Najma akitokea Saudi Arabia.Anadai kwamba mume wake anaitwa Abu Zalawi ana namba zangu

za simu na jana alinipigia mara tatu lakini simu yangu haikuwa ikipatikana.Nilistuka na kumjibu kwamba simfahamu huyo Abu Zalawi na wala sina rafiki mwenye jina hilo.Najma aliendelea kusisitiza kwamba huyo mume wake ameziandika namba hizo katika kitabu chake cha anuani mbali mbali na ameandika jina Ruby.Baadae nikampigia tena nikamuomba anitumie picha ya huyo mume wake nimuone yawezekana nikawa ninamfahamu akaniomba nimpe muda kidogo na

nilipompigia tena akadai kwamba hajaziona picha atanitumia baadae.Gosu hii imenistua kidogo.Sina rafiki yeyote Saudi Arabia na kinachonipa hofu zaidi ni kwamba mtu huyo ananifahamu na ana namba zangu hizi ninazotumia hapa Tanzania.Nimeogopa Gosu Gosu ninahisi labda uingereza wakawa wamegundua kwamba sikufariki katika ile ajali ya ndege na wanaanza kunichunguza” akasema Ruby

“Ruby nashauri kitu kimoja kifanyike.Tumtafute

huyo Abu Zalawi ni nani?Wewe ni mtaalamu sana wa mambo hayo.Yawezekana akawa ni mtu unayemfahamu” akasema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu umenipa wazo zuri sana.Ngoja nimtafute nimfahamu ni nani huyo Abu Zalawi” akasema Ruby na kutoka katika ofisi ya Gosu Gosu akarejea ofisini kwake na haraka haraka akaingia katika program maalum ya kutafuta watu akaanza kumtafuta Abu Zalawi.Ilichukua dakika tatu program ile kumaliza kutafuta na kutoa majibu.Akafungua

taarifa aliyopewa na program yake na kukuta kuna majina zaidi ya mia mbili ya Abu Zalawi.

“Watu wengi sana hawa.Ni yupi kati ya hawa ambaye ananifahamu? Halafu mbona karibu wote wanaonekana kuwa na asili ya kiarabu?akajiuliza Ruby kisha akaanza kuwapitia mmoja mmoja akitafuta kuona kama kuna mmoja anaweza akamfahamu katika wale.Ghafla alihisi kama macho yake yamemdanganya.Akafikicha

macho ili aone tena kile alichokiona katika kompyuta yake

“No ! This is not true ! Haiwezekani ! akasema Ruby kisha akainua simu na kumpigia Gosu Gosu akamtaka aende haraka sana ofisini kwake.Haikuisha dakika moja Gosu Gosu akawa ameingia ofisini kwa Ruby

“Kuna nini Ruby? Akauliza Gosu Gosu baada ya kumkuta Ruby amesimama mbali na kompyuta yake.Alionekana kama vile anaiogopa kompyuta ile

“Kuna nini Ruby?Mbona uko mbali na kompyta yako? Akauliza Gosu Gosu lakini Ruby hakumjibu

“Kumetokea nini Ruby?akauliza Gosu Gosu huku akiisogelea kompyuta ya Ruby,akastuka baada ya kuiona picha ya Mathew.

“That’s him ! akasema Ruby

“Mathew ?

“Ndiyo.Ni yeye aliyekuwa ananitafuta hiyo jana” akasema Ruby huku michirizi ya machozi ikionekana mashavuni

“Ruby sijakuelewa” akasema Gosu Gosu

“Hujaelewa nini Gosu Gosu?Nilimtafuta Abu Zalawi na yametokea majina zaidi ya mia mbili nikaanza kupitia jina moja baada ya lingine na kumkuta Mathew naye akifahamika kwa jina hilo la Abu Zalawi.Taarifa zinaonyesha kuwa ni raia wa Saudi Arabia” akasema Ruby

“Mathew amepata uraia wa Saudi Arabia? Gosu Gosu akauliza

“Ndiyo.Ana uraia wa Saudi Arabia na kama haitoshi tayari

ana mke ambaye ni Najma Yule aliyenipigia simu akitaka kunifahamu mimi ni nani” akasema Ruby na kuanza kuwaga machozi

“Ruby ! Ruby ! akasema Gosu Gosu huku akimtikisa Ruby aliyekuwa ameinamisha kichwa chake akilia

“Kwa nini Mathew amenifanyia hivi? Kwa nini hakuniweka wazi kwamba ana mke na familia nyingine huko Saudi Arabia?akasema Ruby

“Nisikilize Ruby”

“Nimeumia sana Gosu Gosu kwa hiki alichonifanyia

Mathew.Ndiyo maana aliniambia kwamba akiondoka nisijaribu kumtafuta kwani alijua nitafahamu kuwa yuko Saudi Arabia na tayari ana mke ! akasema Ruby

“Ruby sikiliza.Naomba nikiri kwamba hata mimi mwenyewe nimestuka sana kwa hiki nilichokiona lakini ni mapema sana kusema chochote kuhusu jambo hili.Ninamfahamu Mathew Mulumbi kama ameamua kuchukua uraia wa Saudi Arabia basi ni kwa sababu maalum.Lazima kuna kitu

anakifanya kule na ndiyo maana alikutaka usimtafute pindi atakapokuwa ameondoka.Siku zote Mathew amekuwa ni mtu wa kuona mbali mara mbili yetu hivyo naamini kabisa kwamba hayuko huko Saudi Arabia kustarehe lazima kuna kitu anakifanya.Hata huyo mwanamke ambaye yuko naye huyo aliyejitambulisha kuwa mke wake nina uhakika mkubwa ni sehemu ya mipango yake.Nimekuwa naye karibu kwa muda mrefu kidogo na nimebahatika kujua

namna anavyoendesha mambo yake.Alikuahidi kwamba atarejea amini hivyo.Mathew Mulumbi hutembea katika maneno yake.Akisema atarudi basi lazima atarudi tu”

“Gosu Gosu tafadhali naomba usinifanye niamini haya unayoniambia” akasema Ruby

“Naomba uniamini Ruby.Ninamfahamu Mathew vizuri.Anaipenda nchi yake kuliko kitu chochote.Kumbuka alikataa kuchukua uraia wa Ufaransa ili aweze kuishi na familia yake kwa kuwa ana

mapenzi makubwa na Tanzania hivyo kuchukua uraia wa Saudi Arabia si kwa kupenda lazima ipo sababu kubwa.Nimeanza kupata picha kuhusiana na kile ulichonieleza kwamba katika ile operesheni ya kumuua James Kasai na yule gaidi wa IS Mathew alikuwa anawasiliana na mtu kila siku usiku na ulihisi mtu huyo aliyekuwa akiwasiliana naye alikuwa akimpa taarifa mbali mbali kuhusiana na operesheni ile.Nadhani Mathew yuko Saudi Arabia

kimkakati zaidi.Kama jana alikutafuta awasiliane nawe basi lazima atapiga tena simu.Lazima kuna jambo anataka kuwasiliana nawe na ninahisi yawezekana ikawa ni kuhusiana na hizi vurugu zinazoendelea" akasema Gosu Gosu

"Gosu Gosu umeongea kitu cha maana sana.Mathew alipotea kwa miaka mitatu na aliporejea alikuja kwa kazi moja tu ya kummaliza James Kasai.Alikuja akiwa anafahamu kila kitu kilichokuwa kinaendelea hapa

Tanzania na alikuja akiwa ana taarifa zote za kuhusiana na James Kasai.Hakuna aliyekuwa anafahamu kama James Kasai anaishi katika jiji la Kampala maisha ya kifahari.Wengi tulikuwa tunaamini kwamba James Kasai anaishi msituni lakini ni Mathew aliyekuja kutufumbua macho kwamba James haishi msituni.Hakuna aliyefahamu kuhusu ujio wa Khalid Sultan lakini jambo hili alilifahamu Mathew.Baada ya kumaliza kile kilichomleta akaondoka zake.Kitendo cha kunitafuta

kwa wakati huu wa hizi vurugu yawezekana kuna kitu anataka kunieleza pia.Ahsante sana Gosu Gosu kwa kushusha presha yangu ambayo tayari ilikwisha panda.Nilikuwa nawaza mambo mengine kabisa nikasahau kufikiri mambo ya msingi" akasema Ruby

"Imekuwa bahati tumefahamu mahala alipo Mathew lakini kama alivyotaka yeye mwenyewe kwamba asitafutwe hadi pale atakapotutafuta yeye mwenyewe.Kitu cha kujiuliza

je huko Saudi Arabia anafanya kitu gani?

“Nahisi yuko sehemu ambako anapata taarifa nyingi za mambo mbali mbali yanayoendelea duniani.Gosu Gosu ninahisi tayari Mathew anaweza kuwa na taarifa kuhusiana na hiki kinachoendelea Afrika Mashariki.Nahisi hiki kinachoendelea kina nguvu ya kutoka nje ya nchi”akasema Ruby

“Hata mimi nimekuwa nikihisi hivyo hasa ukiliangalia suala hili namna

lilivyoanza.Kuna kile kitu kinaitwa gawanya na tawala.Kumbuka mabeberu walishindwa kuigawanya jumuiya ya Afrika mashariki kwa kumtumia Melanie Davis na yawezekana wameamua kutumia njia hii ya machafuko ili wapate nafasi ya kupenda na kuchota rasilimali.Watu hawa ni wajanja sana na wana mbinu nyingi.Watanzania si watu wa kugombana wao kwa wao lakini sasa hivi wamejikuta katika mapigano ya wenyewe kwa wenyewe.Lazima kuna nguvu

kubwa imetumika hapa si bure” akasema Gosu Gosu

Wakati wakiendelea na mazungumzo mlango wa ofisi ya Ruby ukagongwa akaingia katibu muhtasi wake.

“Rais atatoa hotuba muda wowote kuanzia sasa” akasema Yule katibu muhtasi wa Ruby na haraka haraka Ruby akachukua kitanza mbali akawasha runinga iliyokuwa ukutani.Kulikuwa na matangazo ya moja kwa moja kutokea ikulu ambako Rais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania Dr Fabian Kelelo

alikuwa anatarajia kulihutubia taifa.Tayari ndani ya ukumbi ambao angetumia kuhutubia taifa,viongozi mbali mbali walikwisha wasili na aliyekuwa anasubiriwa ni Rais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania.

Hatimaye mlango ukafunguliwa na Rais Dr Fabian Kelelo akajitokeza akiwa ameongozana na walinzi wake.Kwa kuwa ni yeye tu aliyekuwa akisubiriwa akawataka watu waliokuwa wamesimama waketi na hakupoteza muda akaanza

moja moja hotuba yake.Katika simu janja zote ambazo zilikuwa zimewashwa muda huo ziliunganishwa na hotuba ya Rais kama Ruby na Gosu Gosu walivyokuwa wameshauri

“Ndugu watanzania ambao kwa muda huu mmepata bahati ya kunisikiliza,awali ya yote ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai hadi sasa.Ninapenda pia kuchukua nafasi hii kuwapa pole sana wale wote ambao wamepoteza ndugu zao katika vurugu

zinazoendelea hivi sasa hapa nchini kwetu.Ninawaombea vile vile majeruhi wote uponaji wa haraka.

Ndugu zangu watanzania wenzagu,kabla ya kuanza hotuba yangu naomba niwaeleze kitu kimoja ambacho yawezekana wengi wenu hamkijui.Jina langu naitwa Dr Fabian Jumanne Mkawi Kelelo.Baba yangu Mungu amrehemu aliitwa Jumanne Mkawi Kelelo.Alikuwa mwislamu na alioa wake wawili mama yangu akiwa ni mke mdogo.Mke

mkubwa aliitwa Zamaradi alikuwa ni mwislamu na mama yangu aliitwa Veneranda yeye alikuwa mkristu.Kwa mama yangu mimi ni mtoto wa tatu kuzaliwa,nina kaka zangu wawili na ninao pia wadogo zangu wawili.Kaka zangu walioniangulia ni waislamu wakifuata dini ya baba na mimi nilifuata dini ya mama,hata wadogo zangu pia walifuata dini ya mama.Kwa miaka yote hakujawahi kutokea mgogoro wowote ndani mwetu huku kila mmoja akiheshimu dini ya

mwenzake.Baba yangu aliheshimu sana dini ya mama halikadhalika mama aliheshimu sana dini ya baba.Sisi watoto pia tuliheshimiana na kupendana na hakuna aliyedharau dini ya mwenzake.

Nimeamua kuanza kwa kuwapa mfano huu wa familia nilikotoka lakini naamini zipo familia nyingi za aina hii na wanaishi kwa amani.Lengo langu ni kutaka kuwaonyesha kwamba kwa miaka mingi watanzania tumekuwa tukiishi kama ndugu moja licha ya

utofauti wetu wa dini.Wakristu,waislamu na waumini wa dini nyingine tumekuwa tukiheshimiana na kuishi kwa upendo mkubwa.Mara kadhaa kumeibuka watu au vikundi vya watu wa dini moja wakikashifu au kutoa matamshi ya kuudhi waumini wa dini nyingine.Kila pale kulipotokea mikwaruzano yoyote baina ya dini zetu viongozi wa dini walikaa wakazungumza na kuyamaliza na amani ikatamalaki.Nini kimetokea sasa hivi hadi

tumefikia hapa tulipofika? Nani katufikisha hapa? Najua kwa sasa ni vigumu kupata majibu ya maswali haya lakini lazima tujiulize maswali haya na tukipata majibu tutajua nini kimetufikisha hapa.

Dunia nzima inashangaa nini kimetokea Tanzania? Hii ndiyo nchi ambayo kwa miaka mingi imekuwa ni kioo cha amani.Tanzania imekuwa ni kimbilio la watu kutoka nchi zile ambazo amani imetoweka.Nini kimepelekea kuipoteza amani yetu? Ndugu zangu maswali ni mengi sana

ya kujiuliza kwa nini tumefika hapa tulipofika.Tumeipoteza amani yetu ambayo imetunzwa kwa miaka mingi na sasa tunatumia gharama kubwa kuisaka tena amani....

Wakati hotuba ya Rais ikiendelea,katika ofisi ya Ruby akaingia Pamela akiwa na kompyuta mpakato

“Pamela kuna kitu umekipata?

“Ndiyo mkurugenzi” akasema Pamela na Ruby akapunguza sauti ya runinga wakaenda mezani

“Simu ya Karim haipatikani tena imezimwa.Tumejaribu kuiwasha kwa mbali lakini haipatikani na inawezekana tayari amekwisha toa betri”

“Bastard ! akasema Gosu Gosu

“Lakini tumepata mawasiliano ya Karim ya siku saba kabla ya kuanza kwa machafuko.Tumefahamu pia kwamba mara ya mwisho aliitumia simu yake akiwa katika nyumba hii hapa” akasema Pamela na kumuonyesha Ruby mahala

alipokuwepo Karimu mara ya mwisho alipoitumia simu yake

“Tumefanikiwa pia kuipata namba ya simu aliyowasiliana nayo mara ya mwisho na namba hiyo imesajiliwa kwa jina la Denis Sambale.Tumemfuatilia huyu mtu ni mfanya biashara anaishi jijini Tanga” akasema Pamela

“Good job Pamela”akasema Ruby

“Kazi imeanza.Tayari tumepata sehemu ya kuanzia.Itanilazimu kuchukua timu na kuwahi mahala hapo

alipokuwa Karim kuanza uchunguzi” akasema Gosu Gosu

“Hapana Gosu Gosu.Ni hatari kubwa huko nje.Tutatuma kikosi chetu cha makomando wa idara watakwenda mahala hapo na tutawafuatilia kwa kutumia drone zetu tutajua kila kinachoendelea mahala hapo”

“Ruby..”

“Gosu Gosu nimekwisha sema hauendi huko mtaani hali si nzuri.Ngoja tutume kikosi chetu cha makomando ambao watavamia nyumba

hiyo na kufanya uchunguzi na kama Karim atakuwepo hapo basi ataletwa hapa kwa mahojiano.Naomba tusiwe na mjadala katika hilo”

“Sawa Ruby” akasema Gosu Gosu na bila kupoteza muda Ruby akampigia simu mkuu wa kikosi cha makomando cha SNSA ambao walikuwa wamepiga kambi katika makao maku ya SNSA kuimarisha ulinzi akamtaka wakutane katika chumba maalum cha mipango.

“Gosu Gosu usinielewe vibaya lakini wewe mwenyewe

unaona namna hali ilivyo huko mitaani.Siwezi kukuacha ukaenda huko.Hawa makomando tunaowatuma watafanya kazi nzuri.Wewe ni mtu mkubwa kwa sasa unatakiwa upumzike na uwe ukitoa maelekezo tu.Haya mapambano tunawaachia vijana” akasema Ruby na Gosu Gosu akatabasamu

“Nimekuelewa Ruby” akasema Gosu Gosu kisha wakatoka na kuelekea katika chumba cha mipango ambako tayari kikosi cha makomando nane walikuwa wamefika.

“Habari za asubuhi ndugu zangu” Ruby akawasalimu kisha akaelekea katika runinga iliyokuwa mbele ya chumba kile.

“Kuna kazi ndogo imejitokeza ndugu zangu” akasema Ruby na kubonyza kitanza mbali na katika runinga ikaonekana picha ya Karim Abdallah

“Anaitwa Karim Abdallah.Huyu ni mwanasiasa ambaye anaongoza chama cha upinzani.Ni chama kidogo kisicho na uwakilishi bungeni lakini ni chama ambacho

kimekuwa kikijihusisha na matukio mbali mbali ya uchochezi.Chama hiki kimekuwa kikitoa matamko mbali mbali yenye nia ya kujenga chuki kwa wananchi dhidi ya serikali.Wakati vugu vugu la machafuko yanayoendelea hivi sasa lilipoanza,Karim aliandika katika ukurasa wake wa twitter ujumbe wa uchochezi na kuufuta haraka.Tunataka kumuhoji kuhusiana na ujumbe ule aliouandika ambao ulikuwa ujumbe wa kujenga chuki baina ya waumini wa

dini ya kikristu na kiislamu.Tuna wasiwasi yawezekana machafuko haya yanayoendelea hivi sasa yana chmbe chembe za kisiasa ndani yake" akasema na kubonyeza tena kitanza mbali na picha nyingine ikajitokeza

"Tumefuatilia mawasiliano yake lakini simu yake imezimwa lakini mara ya mwisho alitumia simu yake akiwa katika nyumba hii hapa pichani" akasema Ruby na kuwaonesha ila picha

"Mnakwenda kuvamia nyumba hii na kama Karimu

yuko humo basi achukuliwe na aletwe hapa kwa mahojiano.Yeyote atakayekuwemo ndani ya nyumba hiyo achukuliwe kwani lazima atakuwa akifahamu kuhusu Karim.Jambo la kuzingatia machafuko ni makubwa sana huko nje hivyo basi yeyote atakaye jaribu kuwashambulia mtajibu haraka sana ! akasema Ruby kisha wakauliza maswali kadhaa halafu wakatoka kwenda kujiandaa.Ruby na Gosu Gosu wakaenda kuzungumza na wafanyakazi

ambao karibu wengi walikuwa wanaendelea kutazama hotuba ya Rais.

“Tusikilizane ndugu zangu” akasema Ruby

“Katika uchunguzi wa haraka haraka imegundulika kwamba simu ya Karim Abdallah imezimwa lakini mara ya mwisho aliitumia simu hiyo akiwa katika nyumba hii hapa” akabonyeza kitanza mbali na nyumba ikaonekana runingani.

“Katika nyumba hii ndimo Karim alitumia simu yake mara ya mwisho na

aliwasiliana na mtu anaitwa Denis Sambale ambaye ni mfanya biashara wa jiji la Tanga.Kikosi chetu cha makomando kinaelekea katika nyumba hiyo hivi sasa kuchunguza na kama wakifanikiwa kumpata Karim ataletwa hapa kwa ajili ya mahojiano.Nataka tujielekeze huko kwa sasa.Drone zetu zielekezwe katika misheni hii ndogo ili tuweze kuhakikisha watu wetu wanakwenda na kurejea wakiwa salama” akasema Ruby na zoezi likaanza mara moja.

Makomando nane wakapanda katika helkopta na kuondoka kuelekea katika nyumba wanayokwenda kuichunguza.Tayari drone moja ilikwisha elekezwa katika nyumba ile ambayo makomando walikuwa wanakwenda na hakukuonekana mtu yeyote kwa nje.Milango na madirisha vyote vilikuwa vimefungwa.

Ilichukua dakika kumi na mbili kwa helkopta iliyowabeba makomando kufika katika nyumba ile.Hali ilikuwa shwari maeneo yale

hakukuwa na makundi ya wananchi waliokuwa wanapambana.Makomando wale walihakikishiwa toka ofisi kuu waliokuwa wanalichunguza eneo lile kwa drone kuwa ni salama na wanaweza kushuka.Hakukuwa na sehemu ya helkpota kuweza kutua hivyo makomando wakaanza kushuka kwa kutumia kamba na waliposhuka wote helkopta ikabaki angani ikiwasubiri wamalize jukumu lao.

Haraka haraka mlango wa mbele wa nyumba ukavunjwa

wakaingia ndani.Sebuleni hakukuwa na mtu yeyote na nyumba ilikuwa kimya.Walipita katika vyumba vyote lakini hakukuwa na mtu yeyote.

“Hakuna mtu yeyote ndani ya hii nyumba,narudia tena hakuna mtu yeyote ndani ya hii nyumba” mkuu wa kikosi kile cha makomando akawajulisha SNSA.

“Kuna kitu chochote mmekiona humo ndani kinachoweza kutusaidia? Ruby akauliza

“Katika vyumba vya kulala tumekuta makabati yako wazi na hakuna nguo hata moja ndani yake na inaonyesha kwamba waliokuwa wanaishi humu waliondoka haraka haraka” akasema kiongozi Yule na kugeuka baada ya mmoja wa makomando kumfuata na albamu la picha akalifungua akapitia picha kadhaa kisha akasema

“SNSA inaonekana hapa ni nyumbani kwa Karim kwani tumekuta kuna albamu la picha zake na familia yake”

“Ahsante kamanda kwa kazi nzuri.Mnaweza kurejea ofisini” akasema Ruby

“Tumemkosa huyu jamaa.Yuko wapi? Akauliza Ruby

“Kitendo cha kuondoka kwake kinazidi kutufanya tuendelee kumchimba zaidi.Baada ya kumkosa Karim zoezi sasa linahamia Tanga kwa Denis Sambale ambaye alipigiwa simu na Karim” akasema Gosu Gosu

“Ninakwenda Tanga.Nitaongozana na kikundi cha makomando”

akasema Gosu Gosu na Ruby akamtazama akataka kusema kitu

“Najua unachotaka kukisema Ruby lakini safari hii ninakwenda Tanga na timu ya makomando kumtafuta Denis Sambale.Usihofu Ruby nitakuwa salama” akasema Gosu Gosu

“Gosu Gosu ninasita sana kukuruhusu uende huko lakini ..”

“Ruby niruhusu niende nitakuwa salama.Mimi ni mwanajeshi na siwezi kuogopa.Nitaongozana na

kikosi cha makomando kwenda Tanga kumfuatilia huyo mtu.Tutashirikiana pia na watu wa ofisi yetu ya Tanga” akasema Gosu Gosu na Ruby akatafakari kwa muda halafu akasema

“Gosu Gosu kuna watu wetu wako Tanga.Tutawatuma kwenda kumtafuta huyo mtu aliyewasiliana mara ya mwisho na Karim” akasema Ruby

“Tanga ndiko kuna machafuko makubwa zaidi na inahitaji watu wenye uzoefu wa mapigano kama mimi ! akasema Gosu Gosu

“Gosu Gosu watu hawa tuliwaamini kwamba wanaweza kazi ndiyo maana tukawakabidhi ofisi.Hawakupewa ofisi bila kukidhi vigezo.Wamepitia mafunzo na wanafahamu nini wanatakiwa kufanya.Hatuwezi kutuma watu kutoka Dar es salaam kwenda Tanga wakati kule kuna timu ya watu wetu.Tutawatumia hao watu wetu kumsaka Denis Sambale” akasema Ruby halafu wakatoka kwenda kuzungumza na wafanyakazi.

“Kama mlivyoshuhudia makomando wetu wamefika katika nyumba ambayo imegundulika ni makazi ya Karim Abdallah lakini hajapatikana inaonekana yeye na familia yake wametoweka na hakuna ajuaye wameelekea wapi.Baada ya kumkosa Karim sasa tunageukia kwa mtu ambaye aliwasiliana naye mara ya mwisho anaitwa Denis Sambale.Huyu ni mfanya biashara wa jiji la Tanga.Tunaamini yawezekana kuna kitu anakifahamu kuhusiana na mahala alipo

Karim.Tuna watu wetu walioko Tanga tutawatumia kumsaka huyu Denis Sambale.Nataka tufahamu mahala alipo huyu mtu na kama simu yake imewashwa tumfuatilie na kuwasiliana na watu wa Tanga ili wamkamate.Tumchimbe na tujue watu anaowasiliana nao ni akina nani.Nataka zoezi hilo likamilike kwa haraka ili tuweze kuwasiliana na watu wa Tanga" akasema Ruby na mara moja kazi ikaanza ya kumchunguza Denis Sambale

****

Timu ya watu wa SNSA walioko jijini Tanga iliwasili kaika nyumba ambayo kumbu kumbu zinaonyesha ndiko alipokuwa Denis Sambale mara ya mwisho alipotumia simu yake kwa mawasiliano.Walipofika mahala walipoelekezwa walipatwa na mshangao baada ya kukuta nyumba hiyo ikiwa imeteketea kwa moto na kubaki gofu.Kila kilichokuwamo ndani ya nyumba hiyo kiliteketea

Kwa mujibu wa uchunguzi wa SNSA,ilibainika kwamba mtu wa mwisho Denis kuwasiliana naye alikuwa ni Augustin Kawala ambaye naye simu yake haikuwa inapatikana.Timu ya watu wa SNSA walielekea mahala alipokuwapo Augustin mara ya mwisho alipotumia simu yake.Nyumba ilikuwa na geti lililofungwa kufuli kwa nje kuashiria kwamba hakukuwa na mtu ndani.Wakavunja kufuli na kuingia ndani ya nyumba ile.Mara tu walipouvunja mlango wa

sebuleni walikutana na harufu kali ya uozo.Kwa tahadhari kubwa wakafuatilia harufu ile ilikotoka na kukuta katika chumba kimoja mwanamke mmoja akiwa amelala kitandani akiwa tayari ameanza kuharibika.Kifuani alikuwa amechomwa na kisu kikubwa.Ilionekana kulikuwa na ugomvi kabla ya mwanamke Yule kuuawa kwani vitu vilitawanyika hovyo mle chumbani.Kwa tahadhari kubwa kiongozi wa timu ile ya SNSA akabandika karatasi Fulani katika mpini wa kisu na

kuibandua kisha akaimulika kwa tochi na zikaonekana alama za vidole zilizokuwa katika mpini ule wa kisu.

Katika uchunguzi wao walikuta kuna picha kadhaa zikimuonyesha mtu aliyevaa mavazi ya kichungaji zikiwa zimebandika ukutani na katika picha nyingine alionekana mwanamke Yule aliyeuawa akiwa na Yule mchungaji ilikuwa ni siku ya harusi yao.Walikusanya kila walichoona kingeweza kuwafaa kisha wakaondoka kurejea katika ofisi yao.Karatasi ile

iliyokuwa na alama za vidole kutoka katika ule mpini wa kisu alichochomwa Yule mwanamke waliyemkuta katika nyumba ya Augustin Kawala ikaingizwa katika kompyuta na alama zile zikatumwa ofisi kuu ya SNSA Dar es salaam.

****

Katika chumba cha mipango ofisi kuu ya SNSA Dar es salaam,Ruby akiwa na Gosu Gosu msaidizi wake pamoja na viongozi kadhaa wa idara mbali mbali zilizomo

ndani ya SNSA walikutana kufuatia ripoti waliyoipata kutoka kwa watu wao walioko Tanga.

“Muda mfupi uliopita nimepokea taarifa kutoka Tanga.Tuliwaelekeza watu wetu kule kumfuatilia Denis Sambale lakini walipofika katika nyumba ambayo tunaamini ni makazi yake walikuta nyumba hiyo ikiwa imeteketea kwa moto” akasema Ruby na kuwaonyesha picha katika runinga kubwa za namna

nyumba ile ilivyoteketea na kubaki gofu

“Denis Sambale mara ya mwisho aliwasiliana na Augustin Kawala,watu wetu wakamfuata huyo Augustin ambaye naye simu yake haipatikani na walipofika katika nyumba ambayo alikuwepo alipowasiliana na Denis watu wetu wamekuta nyumba ikiwa imefungwa wakavunja mlango wakaingia ndani na hiki ndicho walichokikuta” akasema Ruby na kuwaonyesha picha za Yule mwanamke aliyekutwa

ameuawa kwa kuchomwa na kisu kifuani

“Watu wetu walichukua alama za vidole kutoka katika mpini wa kisu alichochomwa mwanamke huyo .Watu wa idara ya alama wamezifanyia kazi alama hizo na haya ndiyo majibu waliyoyapata.Katika alama zilizokutwa kwenye hicho kisu kuna alama za vidole za mtu huyu hapa” akasema na kubonyeza kitanza mbali na picha ikajitokeza

“Augustin Kawala.Huyu ni mchungaji anayemiliki kanisa la ngome ya ushindi.Katika

alama hizo pia zimekutwa alama za mtu huyu hapa” akasema na katika runinga ikatokea picha ya mwanamke

“Anaitwa Paulina Kawala.Huyu ni mke wa Augustin Kawala.Katika picha zilizotumwa na watu wetu wa Tanga ipo picha inayoonyesha Augustin na Paulina siku ya harusi yao.Kufuatia kukutwa kwa alama za vidole za Augustin katika mpini wa kisu alichochomwa Paulina inaonyesha wazi kwamba huyu jamaa anahusika katika mauaji ya mke wake.Hii ndiyo hali

iliyokutwa chumbani” akasema Ruby na kuonyesha picha za namna vitu vilivyovurugika chumbani.

“Inaonekana kulikuwa na ugomvi chumbani na kisha Paulina akachomwa kisu.Mtu wa kwanza ambaye tunamuhisi kuhusika na mauaji hayo ni Augustin Kawala.Hatujui mahala alipo na simu yake imezimwa.Kuna kitu kimoja ambacho naamini mmekigundua katika zoezi hili tulilolifanya leo.Tukianza kwa Karim,ametoweka na hatujui yuko wapi.Mtu wa mwisho

kuwasiliana naye ni Denis Sambale akiwa jijini Tanga.Huyu naye hajulikani alipo na nyumba yake imeteketea kwa moto.Denis naye mtu wa mwisho kuwasiliana naye ni Augustin Kawala huyu naye ametoweka hatujui alipo ila tunaamini huyu alimuua mkewe na akakimbia.Wote hawa mawasiliano yao ya mwisho yamefanywa siku ambayo machafuko yalianza jijini Tanga na wote simu zao hazipatikani.Binafsi nalazimika kuamini huu ni

mtandao ambao una malengo Fulani na ninahisi unahusika kwa namna moja au nyingine na haya machafuko” akanyamaza kidogo halafu akaendelea

“Nilipewa orodha ya watu ambao waliwasiliana na Karim wiki moja kabla ya machafuko kuanza.Katika orodha hiyo kuna mwanasiasa mmoja wa Uganda anaitwa Joshua Lulangwa.Nitazungumza na Rais ili aombe msaada kwa mamlaka za Uganda kuweza kupata taarifa za kuhusiana na huyu mtu.Wakati tukisubiri

msaada huo kutoka kwa wenzetu wa Uganda sisi tutaendelea kuwafuatilia watu wote walioko katika orodha hii ya watu ambao Karim aliwasiliana nao na tutamfahamu kila mmoja wao na kuchunguza kama ana mahusiano yoyote na vurugu hizi.Hakuna kufumba jicho hadi pale tutakapopata chanzo cha vurugu hizi ambazo binafsi ninahisi wanasiasa wanaweza kuhusika" akasema Ruby.Tayari ni saa kumi na mbili kasoro za jioni akampigia simu Rais

akamjulisha kwamba atakwenda kuonana naye jioni ile

WASHINGTON DC – MAREKANI

Inakaribia saa saba za mchana wakati ndege iliyowabeba Habiba Jawad na Mathew Mulumbi ilipowasili katika anga la jiji la Washington DC.Ni safari iliyowachukua takribani saa kumi na nne kutoka Riyadh.

“Mathew imekuwa ni safari ndefu sana na tunakaribia kutua lakini kuna

kitu kimoja nataka kukufahamisha kabla ndege haijagusa ardhi” akasema Habiba

“Nakusikiliza mama”

“Sikupaswa kukwambia lakini wewe ni kijana wangu hivyo lazima nikwambie ili ujiandae.Hawa watu hawakuamini”

“Akina nani? akauliza Mathew

“Hawa tunaokwenda kuonana nao”akajibu Habiba

“Wana haki ya kuwa na wasi wasi nami kwani hawanifahamu na ni mara ya

kwanza tunakutana mimi na wao hivyo hali kama hiyo lazima itokee”akasema Mathew

“Sikiliza Mathew.Tutakaposhuka watakuchukua na kwenda kukupima.Show them who you are !

“Watanipimaje?akauliza Mathew

“Sifahamu lakini lazima upimwe hivyo waonyeshe wewe ni nani.waonyeshe uwezo wako wote ! akasema Habiba lakini Mathew hakuonekana kumuelewa

“Mama nashindwa kukuelewa”

“Mathew sina muda wa kukufafanulia.Sikiliza kile ninachokwambia na ujiandae kwani sikupaswa hata kukueleza chochote kuhusiana na suala hili.Hakikisha hawagundui kuwa umejiandaa” akasema Habiba

“Mama ni ak……” Akataka kusema kitu Mathew lakini Habiba akamzuia

“Mathew sihitaji maswali.Tunakaribia kutua jiandae” akasema Habiba

Ndege ilitua katika uwanja wa kijeshi wa Bollling Airface Base.

“Mathew good lucky” akasema Habiba na kuinuka Mathew akachukua sanduku lake akamfuata Habiba wakaanza kutoka nje.Habiba Jawad alikuwa wa kwanza kushuka ndegeni huku Mathew akimfuaa nyuma yake. Kulikuwa na watu watano wakiwa katika mavazi ya suti na wengine wanne walikuwa katika mavazi ya kijeshi.Wanajeshi wawili wakamsogelea Mathew na

kumtaka asubiri .Habiba Jawad aliyekuwa ameogozana na watu wanne akageuka akamtazama Mathew kisha akaingia katika mojawapo ya magari manne yaliyokuwepo pale uwanjani na magari mawili yakaondoka yakabaki mawili.Baada ya Habiba Jawad kuondoka Mathew akaelekezwa kushuka ndegeni akaongozana na wale wanajeshi wanne ambao wawili kati yao walikuwa na silaha wakaelekea katika gari.Mlango wa pembeni wa gari lile ukafunguliwa na

Mathew akatakiwa kuingia kisha magari yakaondoka bila Mathew kuelezwa chochote

“Mnaweza mkanieleza tunakoelekea? Akauliza Mathew lakini hakuna aliyemjibu

Walikatisha mitaa kadhaa ya jijila Washington halafu wakaingia katika nyumba moja ambayo kuta zake zote zilikuwa zimeeneza majani ambayo huota kufuata ukuta.Nyuma yote ilikuwa ya kijani kufuatia rangi ya majani yale isipokuwa bati ambalo lilikuwa jekundu.Mathew

akatakiwa kushuka garini akaongozwa na wanajeshi wale wanne kuingia ndani.Mlangoni kulikuwa na jamaa mmoja aliyekuwa ameva suti nzuri ya rangi ya bluu akafungua mlango na wanajeshi wawili wakatangulia ndani Mathew akafuata nyuma yao kisha wanajeshi wale wawili wakafuata nyuma ya Mathew pamoja na jamaa wengine watano.

“Hapa ni wapi? Yule mama niliyekuja naye ndegeni yuko wapi?akauliza Mathew akionyesha wasiwasi

“Tulia na fuata kile utakachoelekezwa” akasema jamaa mmoja halafu akaenda chumbani na kurejea na nguo akamtaka Mathew avue mavazi yake na avae nguo zile alizomletea.

“Ninapelekwa wapi?akauliza Mathew

“Nimekwambia fanya kile nilichokuelekeza.Vua mavazi yako na uvae mavazi haya”

Mathew akashika nguo zile akazikunjua akazitazama

“Sikiliza Mathew.Tutakaposhuka watakuchukua na kwenda

kukupima.Show them who you are !

Mathew akayakumbuka maneno aliyoambiwa na Habiba Jawad,akazitupa chini zile nguo.

“Sivai mavazi hayo hadi mtakaponieleza wapi mnataka kunipeleka ! akasema Mathew na wale jamaa wakatazamana

“Tafadhali ndugu vaa mavazi hayo uliyopewa,usijitafutie matatizo”Mathew akaelekezwa

“Nimesema sivai mavazi yenu hadi mtakaponieleza

wapi mnanipeleka ! akasema Mathew

“Hii ni mara ya mwisho nakuomba ndugu vua hayo mavazi uliyovaa na vaa mavazi haya uliyoelekezwa kuvaa ! akafoka mmoja wa wale jamaa aliyekuwa amevaa suti ya kijivu

“Hivi ndivyo mnavyowatendea wageni wanaokuja kutembelea nchi yenu?Kwa nini mmenileta hapa?Nimefanya kosa gani? Kuna sheria ya Marekani nimevunja? Akauliza Mathew

kwa ukali na wale jamaa hawakumjibu

“Hamtaki kunijibu? Akauliza tena Mathew

“Kama hamna jibu la kunipa naomba tafadhali mniache niende zangu kabla ubalozi wangu haujaanza kunitafuta ! akasema Mathew na jamaa aliyevaa suti ya kijivu akawapa ishara wale wanajeshi

“Hebu mkaribisheni Marekani ! akasema Yule jamaa na wanajeshi wawili ambao walikuwa wamejaza mikono yao wakamsogelea Mathew.Mmoja wa wale

wanajeshi akamtandika kichwa Mathew akaenda chini akahisi nyota kwa kichwa kile kizito.

“Waonyeshe wewe ni nani.Waonyeshe uwezo wako wote ! Mathew akayakumbuka tena maneno ya Habiba Jawad akiwa ameanguka chini

Akiwa pale chini mmoja wa wale wanajeshi akainua mguu wake kwa lengo la kumkanyaga lakini tayari Mathew alikwisha kiona kitendo kile akaukwepa mguu wa Yule mwanajeshi ambao ulipiga ardhi kwa kishindo na

Mathew akajigeuza na kumkata mtama Yule mwanajeshi akaanguka mzima mzima sakafuni na kutoa kishindo.Kwa kutumia miguu yake akaibinua meza ndogo iliyokuwa karibu yake akaidaka na kisha akasimama kwa kasi na kumpiga nayo mmoja wa wale wanajeshi ikampeleka chini.Jicho la Mathew lililogeuka kama kinyonga lilimuona mwanajeshi mmoja akimjia nyuma yake akageuka na kumtandika teke zito la uso halafu akapanda juu ya sofa na

kumrukia mwanajeshi wa nne mateke mawili mfululizo kifuani akaanguka chini.Yule mwanajeshi aliyepigwa na meza ndogo tayari alikwisha inuka na mkononi alikuwa ameshika ubao uliotoka katika ile meza aliyopigwa nayo na kwa nguvu akaurusha ubao ule kumuelekea Mathew lakini tayari alikwisha uona ule ubao akaukwepa ukampiga jamaa aliyekuwa amesimama akishuhudia wanajeshi wao wakitembezewa kipigo kikali.Baada ya kumkosa na ule ubao Yule mwanajeshi

ambaye tayari alikwisha
pandwa na hasira akaruka
mzima mzima kutaka
kumvamia Mathew mahala
alipokuwa amejibanza lakini
Mathew alikuwa mwepesi zaidi
yake akaruka juu na kumuwahi
Yule jamaa akiwa juu na
kumtandika teke zito la kifua
na kumfanya Yule jamaa
aanguke kama furushi.Mathew
akajigeuza na kutua nyuma ya
Yule jamaa aliyepigwa na ubao
ambaye alikuwa amepiga
magoti damu ikimtoka
mdomoni akamkaba kabali
kwa mkono wake wa kushoto

halafu akaiokota bastora ya Yule jamaa iliyoanguka pembeni akamuwekea kichwani.

“Wote inue mikono juu ! Mathew akawaamuru wale jamaa waliovaa suti ambao wote walikuwa wameshika bastora zao wakimuelekezea.

“Namaanisha ninachokisema wote inueni mikono juu ! akasema Mathew kwa ukali lakini wale jamaa bao waliendelea kumuelekezea bastora

“Nitahesabu hadi tatu kama hamtatii nitamtandika

mwenzenu risasi..Moja ! Mathew akaanza kuhesabu

“Mbili ! akaendelea

“Fanyeni anachowaelekeza ! akasema Yule jama aaliyekabwa kabali ambaye alikuwa anapata taabu kuvuta pumzi.

“Wekeni silaha zenu chini na muinue mikono juu ! akaamuru Mathew na taratibu wale jamaa wakaziweka chini bastora zao na kuinua mikono juu kama walivyokuwa wameelekezwa

“Wewe inuka ! Mathew akamuelekezea bastora mmoja

wa wanajeshi akamtaka ainuke akaziokote zile bastora na kumsogezea karibu.Yule mwanajeshi akafanya alivyoelekezwa akaziokota bastora na kumsogezea Mathew halafu akamtaka kuchukua pingu kutoka katika suti zao na kuwafunga mikono.Mwisho akamtaka Yule mwanajeshi ajifunge pingu yeye mwenyewe.Wanajeshi wengine watatu hali zao hazikuwa nzuri wawili walikuwa wamepoteza fahamu na mmoja alikuwa anatoka damu

mdomoni.Mathew alipohakikisha wote wamefungwa pingu akampiga Yule jamaa pigo kichwani akaanguka na kupoteza fahamu akachukua bastora mbili akazifutika kiunoni halafu akatoka mle ndani akaufungua mlango wa mojawapo ya gari akaingia ndani akaliwasha.

“Ninaelekea wapi?akajiuliza

“Nitajua pa kuelekea ngoja kwanza niondoke mahala hapa” akawaza Mathew na kugeuza shingo akatazama

nyuma ili kugeuza gari lakini akasikia muunguruo wa helkopta iliyofikan a kusimama juu ya ile nyumba.Mara akasikia mivumo ya risasi na gari ikabonyea chini matairi yote yalipigwa risasi.

“Bastard ! akafoka Mathew huku akiupiga usukani kwa hasira na kutokea upande wa pili ikatokea tena helkopta ya pili ambayo kama ile ya kwanza mlangoni alikuwepo jamaa aliyekuwa na bunduki kubwa.Wakati Mathew akitafakari geti likafunguliwa

na gari mbili zikaingia.Mathew akaelekeza macho ukutani na kuwaona watu wanne wenye bunduki wakiwa wamezielekeza kwake.Wale jamaa walioingia na magari wakashuka na mmoja wao akatumia kipaaza sauti kumtaka Mathew ashuke garini.

“Sina ujanja,siwezi kutoka salama mahala hapa.Wako wengi na wamejizatiti kwa silaha” akawaza Mathew na kufungua mlango wa gari.Bunduki zote zikaelekezwa katika lie

gari.Akatoa mguu akaushusha chini taratibu,akatoa na mwingine halafu akatoa mkono wa kwanza akauonyesha ukiwa mtupu akatoa na mkono wa pili akauonyesha ukiwa mtupu halafu akashuka garini na kuinua mikono juu.Haraka haraka na kwa tahadhali watu wanne wakamsogelea na kuanza kumpeua hakuwa na bastora zote aliziacha garini,akafungwa mikono kwa pingu na kufunikwa mfuko kichwani akaingizwa garini na kuondoka eneo lile.

****

Gari lilisimama mlango ukafunguliwa na Mathew akashushwa.Watu wale walifanya mambo yao kimya kimya bila maongezi hivyo hakujua kulikuwa na watu wangapi eneo lile lililokuwa na ukimya mkubwa.Aliingizwa katika jumba lililokuwa na ubaridi mwingi.Mlango wa mojawapo ya chumba katika jumba lile ukafunguliwa na Mathew akaingizwa ndani ya chumba hicho akaketishwa

kitini halafu akafunguliwa pingu alizokuwa amefungwa mikononi akafungwa katika pingu nyingine zenye mnyororo zilizounganishwa na chuma kilichokuwa juu ya meza akaachwa hapo na watu wale wakaondoka.

“Nini wanataka kukihakiki kwangu hawa jamaa ambao Habiba amesema wananifanyia majaribio? Ngoja nifuate maelekezo ya Habiba kwamba niwaonyeshe mimi ni nani” akawaza Mathew

Ndani ya chumba kimoja kizuri katika jengo moja

lililokuwa kati kati ya jiji la Washington watu tisa walikuwa wameyaelekza macho yao katika runinga kubwa wakifuatilia kile kilichokuwa kinaonekana pale runingani.Katika runinga ile alionekana Mathew Mulumbi akiwa ndani ya chumba alimofungwa akiwa na mfuko kichwani

Mathew aliinamisha kichwa upande mmoja na alionekana kama vile anauma kitu kwa meno yake.Baada ya dakika tatu akainamisha kichwa mezani na kusogeza

kiganja cha mkono karibu na mdomo akachukua kitu ambacho hakikuweza kuonekana vizuri halafu akaanza kuchokonoa pingu ya mkono wa kushoto ikafunguka akavua ule mfuko aliofunikwa kichwani halafu akaifungua na ile ya mkono wa kulia akawa huru.

“Habiba huyu jamaa ni Gaidi au ni jasusi?akauliza Edward Murphy

“Huyu ni gaidi” akajibu Habiba

“Anafanya mambo ya kushangaza ambayo magaidi

wengi hawawezi kuyafanya.Umemtoa wapi huyu?akauliza Robin Ross.Kabla Habiba hajajibu Mathew akaelekea mlangoni wote wakayaelekeza macho runingani kutazama anachotaka kukifanya.Mathew akauchunguza ule mlango akagundua ni mlango unaofunguliwa kwa kutumia kadi ya kielektroniki.Akavua kiatu chake cha mguu wa kulia akang'oa kisigino halafu akang'oa kipande cha chuma kisha akatoa bisibisi ndogo na vitu vingine vidogo

vidogo.Wote mle ndani ya chumba wakabaki wanashangaa

Mathew akafungua sehemu ya kupitisha kadi ya kielektroiki ya kufungulia ule mlango.Kulikuwa na nyaya kadhaa katika kiboksi kile akazichunguza halafu akakunjua kisu kidogo sana ambacho alikitoa katika kisigino cha kiatu akakata nyaya kadhaa akazichuna na kuunganisha na mara mlango ukafunguka

“Yawezekana wakawa wananitazama muda huu

ninachokifanya.Hizi ni salamu zao” akawaza Mathew halafu akatoka ndani ya kile chumba akafuata varanda hadi alipokuta mlango uliokuwa umefungwa kwa nje.Pembeni yake kulikuwa na chumba ambacho mlango wake ulikuwa wazi.Akaingia ndani ya kile chumba mara mlango wa kile chumba ukajifunga halafu akasikia hatua za mtu akisogelea ule mlango wa kile chumba alimo akajiandaa kukabiliana na yeyote atakayeingia mle na mara akaona moshi ukipenya chini

ya mlango.Taratibu akaanza kuhisi macho yanapoteza nguvu ya kuona akaanguka chini na kupoteza fahamu.

****

Mathew alirejewa na fahamu na kujikuta akiwa amelazwa kitandani.Ndani ya chumba kile kizuri kulikuwa na akina dada wawili warembo wakiwa wameketi katika sofa lililokuwamo mle chumbani.Taratibu akajiinua na kukaa wale akina dada wenye tabasamu murua

wakamsogelea na kuketi kitandani mmoja wao akamsugua sugua mgongoni

“Pole sana.Unajisikiaje sasa? Kuna sehemu yoyote inauma?akauliza Yule mwanadada kwa sauti nyororo

“Kichwa kinaniuma sana” akajibu Mathew na Yule mwanadada akampa vidonge viwili akameza.

“Naitwa Sophia mwenzangu anaitwa Emily.Wewe jina lako nani? Akauliza Sophia aliyeonekana mzungumzaji sana

“Abu Zalawi”

“Abu Zalawi karibu sana Washington DC.Pole kwa yote yaliyotokea na sasa nakuomba uingie bafuni ukaoge halafu tuondoke”

“Mnanipeleka wapi?

“Sikiliza Abu Zalawi tumepewa maelekezo utakapozinduka tukupeleke sehemu hivyo tusipoteze muda oga vaa mavazi pendeza” akasema Sophia na Mathew akaingia bafuni akaoga kisha akatoka na kukuta kuna suti nzuri nyeusi kitandani pamoja na viatu vizuri vyeusi akavaa.Hakuwa na haja ya

kujitazama katika kioo kwani suti ile ilimkaa vyema.Akagonga mlango Sophia na Emily wakaingia.

“Mbona hujavaa tai?akauliza Sophia

“Sipendelei kuvaa tai”

“Sogea hapa karibu” akasema Sophia na kumfungia Mathew tai kisha akampa mfuko ili auvae kichwani.Sura ya Mathew ikabadilika

“Najua hupendi Abu Zalawi lakini lazima uvae.Hizi ndizo taratibu” akasema Sophia

“Tafadhali vaa Abu Zalawi” akasisitiza Sophia na Mathew akauvaa mfuko ule wakamuongoza kutoka ndani ya ile nyumba hadi katika gari wakaondoka

Baada ya mwendo wa dakika zaidi ya thelathini hatimaye gari ikasimama na milango ikafunguliwa Mathew akashushwa na akahisi kuna mikono mizito ya mwanaume ikimkamata mkono wake na kumuongoza kuelekea ndani.Waliingia katika lifti kisha wakashuka na kutembea kidogo akasikia mlango

ukifunguliwa wakaingia ndani ya chumba na Mathew akaenda kuketishwa kitini halafu akatolewa ule mfuko kichwani.Ndani ya chumba kile kikubwa na kizuri kulikuwa na meza kubwa ya duara na watu wasiopungua kumi na tano walikuwa wameizunguka meza ile na mmoja wao alikuwa ni Habiba Jawad.Mathew akashusha pumzi baada ya kumuona Habiba

“Abu Zalawi napenda kuchukua nafasi hii kukukaribisha sana

Washington DC” akasema mzee mmoja aliyejitambulisha kwa jina la David Walker.

“Ahsante” akajibu Mathew.

“Kuna mambo yametokea ambayo yamekushangaza.Ulichukuliwa uwanja wa ndege na kupelekwa mahala usipopafahamu na hukujua kwa nini.Kilichotokea ni utaratibu wetu wa kuwapokea wageni wanaofika kwa mara ya kwanza na vile vile tulikupitisha katika mtihani mdogo kupima uwezo

wako.Kila mtu ambaye huwa na ana mahusiano na sisi hupimwa uwezo wake katika mambo mbali mbali.Wengine huwapeleka gerezani au katika nyumba za mateso kuwapima namna wanavyoweza kukabiliana na hali ngumu.Kwako pia ilipangwa iwe hivyo lakini kwa umahiri uliouonyesha nina furaha kukujulisha kwamba umefaulu jaribio kwa alama za juu sana.Mambo uliyotuonyesha hatukuwa tena na ulazima wa kuendelea na zoezi la kukupima.Karibu sana

Washington DC” akasema David Walker na Mathew akainamisha kichwa kushukuru

“Namshukuru sana Habiba kwa kunijulisha mapema kile walichokipanga hawa jamaa” akawaza Mathew

“Abu Zalawi kabla ya yote napenda nimpe nafasi Habiba Jawad afanye utambulisho kisha atoe maelezo machache.Karibu Habiba Jawad” akasema David Walker na Habiba jawad akasimama

“Ahsante David” akasema Habiba na kumtazama Mathew

“Kwanza kabisa Abu nataka uwafahamu watu walioko humu ndani kwa majina yao.Tukianzia na mwenyekiti pale anaitwa David Walker yeye tayari amekwisha jitambulisha.Anayefuata mkono wake wa kulia ni Richard Smith,anafuata John Hill,anafuata David Carter,Robert Baker,James Campbell,Michael Torres,Donald Cooper,Brian

Watson.Tukirudi kwa upande wake wa kushoto tunaanza na Jason Brooks,Eric Wood,Jeffery Jenkins,Carl Henderson,Terry Hughes,Willie Simmons ,Wayne Sullivan,Edward Murphy na Robin Ross”Habiba akanyamaza

“Baada ya kuwatambua watu hawa walioko mbele yako sasa nageukia upande wa pili.Aliyeko mbele yenu anaitwa Abu Zalawi.Huyu asili yake ni nchini Misri lakini kwa sasa ni raia wa Saudi Arabia.Anatokea katika kundi

la Ammar Nazari brigades ambalo nimekuwa nikilifadhili pia.Kutokana na umahiri wake ninamtumia kama msaidizi wangu na leo hii nimekuja kumtambulisha kwenu rasmi mumfahamu na kumkabidhi majukumu.Ninamuamini Abu Zalawi.Ni mtu ambaye ni mtiifu kwangu na amenisaidia mambo mengi.Naamini nanyi pia mtamuamini kama mnavyoniamini mimi.Mlichokiona leo hii ni sehemu ndogo tu ya uwezo mkubwa alionao Abu Zalawi.Ni mtu sahihi kwa kazi

ambayo mnataka kumtuma.Sina mashaka naye hata kidogo” akasema Habiba akanyamaza kidogo halafu akaendelea

“Abu Zalawi naamini unajiuliza kwamba hawa walioko mbele yako ambao nimewatambulisha kwako ni akina nani?kwa nini tumekuja hapa?Sikukueleza chochote kuhusiana na safari yetu hii lakini leo ni wakati muafaka wa kuufahamu ukweli” akanyamaza halafu akaendelea

“Unanifahamu kama mfadhili mkubwa wa makundi

mbali mbali ya kigaidi hasa kundi la IS.Naamini umekuwa unajiuliza na si wewe peke bali watu wengi nahata wale ambao ninawafadhili kwamba ninafaidika na nini ninapofadhili ugaidi?Hakuna chochote ambacho ninakipata kutoka kwa magaidi lakini nimekuwa nikitoa mabilioni ya fedha kwa makundi mbali mbali na kufadhili operesheni zao mbali mbali za kigaidi.Ukweli ambao wewe na wengine wote hamuufahamu ni kwamba timu hii unayoiona ndani ya chumba hiki ndiyo

inayofanikisha kila kitu.Mimi ninafanya kazi kwa niaba ya timu hii.Wao ndio walioniwezesha kiuchumi na kuwa tajiri mkubwa na utajiri huo ndio ninaoutumia kufadhili makundi ya kigaidi” akasema Habiba na kumtazama Mathew.

“Nadhani umestuka sana kusikia kwamba Marekani wanafadhili kundi la IS na makundi mengine ya kigaidi.Kuna chochote unataka kukisema? Akauliza Habiba huku akitabasamu.Mathew

akakohoa kidogo halafu akasema

“Nimestuka sana.Sikuwahi kufikiri kitu kama hiki.Sikuwahi kufikiri hata siku moja kama Marekani wanaweza wakafadhili makundi ya kigaidi.IS wamekuwa wakifanya mashambulio mbali mbali duniani na kupelekea vifo vya watu wengi na Marekani imekuwa ikitangaza vita dhidi ya kundi hili na tumeona hatua ambazo imekuwa ikizichukua katika kulikabili kundi hili.Napata kigugumizi kidogo

kulielewa hili jambo.Inawezekanaje IS wakafadhiliwa na Marekani ambao wamekuwa wakipanga mikakati mizito na kutumia fedha nyingi kugharamia operesheni ya kulimaliza kundi hili la IS.Au ni kundi lipi la IS linalozungumzwa hapa? Akauliza Mathew akijifanya kustuka na kutokujua chochote.

“David Walker karibu” akasema Habiba na kukaa akamuachia nafasi David Walker ambaye alitaka kutoa

maelezo kumuelewesha Mathew

“Unalolisema Abu Zalawi ni kweli kabisa kwamba Marekani tumekuwa tukitenga bajeti kubwa kila mwaka kwa ajili ya operesheni za kupambana na ugaidi sehemu mbali mbali duniani na hii inaifanya Marekani kuwa kinara wa kupinga ugaidi duniani.Pamoja na kuwa kinara katika vita hiyo dhidi ya ugaidi duniani lakini kuna upande wa pili wa ambao watu wengi hawaufahamu ni kwamba licha ya kuendesha

vita dhidi ya ugaidi lakini Marekani tunawatumia magaidi hao hao katika mipango mbali mbali yenye maslahi mazito kwa Marekani.Hilo ni jambo ambalo hata wamarekani wenyewe hawalifahamu na si wamarekani pekee hata Rais wa Marekani halifahamu.Ni jambo linalofanywa kwa siri kubwa na timu hii unayoiona humu ndani ndio tunaoshughulika na jambo hilo.Hiki ni kitengo maalum cha siri ndani ya idara ya ujasusi CIA ambacho ni

maalum kabisa kwa ajili ya kushughulika na masuala haya ya mashirikiano na makundi ya kigaidi.Ni kitengo nyeti na cha siri mno kiasi kwamba hata wafanyakazi ndani ya CIA hawafahamu uwepo wake hivyo basi kwa mtu kama wewe kufahamu jambo hili ni kwamba umeaminiwa mno na tumekuamini kwa kuwa umeletwa na Habiba Jawad ambaye ni mwenzetu na ambaye ndiye anayefanya kazi kwa niaba yetu.Sisi hatuwafahamu viongozi wa makundi ya kigaidi na wao

hawatufahamu sisi lakini wanamfahamu Habiba Jawad hivyo basi tunakuamini kama alivyokuamini Habiba na ndiyo maana umeifahamu siri hii na kuanzia leo hii wewe ni mmoja wetu japo baada ya kumaliza mazungumzo yetu utalishwa kiapo.Sasa tugeukie ni namna gani tunayatumia makundi haya ya kigaidi na ni namna gani tunafaidika nayo? akasema David Walker.

“Marekani ni taifa kubwa kiuchumi duniani.Kama nchi tunahitaji malighafi kwa ajili ya kuendesha viwanda vyetu

na kuufanya uchumi wetu uzidi kupaa.Malighafi kubwa ambayo tunaihitaji ni mafuta ambayo kwa kiasi kikubwa dunia nzima inategemea mafuta kutoka nchi za Mashariki ya kati.Kwa bahati mbaya Marekani na nchi azalishaji wakubwa wa mafuta duniani hatuna mahusiano mazuri.Ukiangalia nchi ambayo inatajwa kuwa na mafuta mengi zaidi duniani ni nchi ya Venezuela.Unafahamu mahusiano ya Marekani na Venezuela si mazuri.Nchi nyingine ambazo zina akiba

kubwa ya mafuta ni Saudi Arabia hawa ni washirika wetu.Nchi ya tatu ni Canada,ya nne ni Iran.Hawa hatuna maelewano mazuri nao hata kidogo.Zipo pia nchi kama Iraq,Kuwait,UAE,Urusi na Libya.Kama nilivyosema kwamba nchi nyingi wazalishaji wa mafuta ziko Mashariki ya kati na nyingi kati ya hizo hazina maelewano mazuri na Marekani na hii ni kutokana na kuwaunga mkono Israel.Kuna chuki kati ya Marekani na nchi za kiarabu japo si zote kwani zipo nchi za

kiarabu ambazo ni washirika wetu.Ili tuweze kupata mafuta tunawatumia makundi ya kigaidi katika kuanzisha vita na sisi tunapata nafasi ya kupeleka vikosi vyetu kwa kigezo cha kuwasaka magaidi na kisha huchukua mafuta na kuongeza akiba yetu.Tumekwisha fanya hivyo katika nchi kadhaa sina sababu ya kueleza hapa Habiba atakueleza kila kitu kwa hiyo sababu ya kwanza ya kuwatumia magaidi ni ili kuifanya Marekani kupeleka vikosi vyake katika nchi husika

kwa ajili ya kuchukua mafuta.Naomba nisiendelee zaidi kwa kuwa utaendelea kufahamu taratibu kila kitu kuhusiana na sisi" akanyamaza akanywa maji halafu akasema

"Abu Zalawi baada ya kukufahamisha kwa ufupi kuhusu sisi ni akina nani na majukumu yetu sasa tunaingia katika kile ambacho kimetukutanisha hapa sisi na wewe" David akanyamaza tena halafu akaendelea.

"Tulimuomba Habiba atutafutie mtu mahiri kutoka katika makundi ya kigaidi kwa

ajili ya kazi maalum.Baada ya kufanya uchunguzi wake Habiba amekuleta wewe ambaye ndiye anayeona unafaa kwa ajili ya kazi hiyo na tunaamini Habiba hajakosea kwani ameleta hasa mtu yule ambaye tunamuhitaji.Umetuonyesha uwezo wako tumeridhika na sasa ni wakati wa kukufahamisha kazi gani ambayo tunataka ukaifanye” akanyamaza tena kisha akasema

“Kwa muda mrefu sasa nchi za Iran na Marekani

zimekuwa katika mgogoro mkubwa ambao unahusiana na masuala ya silaha.Iran ikisaidiwa na baadhi ya nchi kubwa imejenga vinu vya nyuklia na inadai kuwa ni kwa ajili ya kuzalisha nishati ya umeme lakini tunaamini mpango wa Iran ni kutengeneza kombora la nyuklia.Huu umekuwa ni mzozo wa miaka mingi na umepelekea nchi ya Iran kuwekewa vikwazo mbali mbali vya kiuchumi.Ni kutokana na mzozo huo ililazimika kuwekeana

mkataba kati ya Iran na nchi za ulala na Marekani wa kutokuendelea na urutubishaji wa madini ya Urani.Marekani ilijitoa katika mkataba huo na Iran imetishia kuendelea na urutubishaji wa madini ya urani.Miaka kadhaa iliyopita tuliwateka wanasayansi wa Iran waliotoka Urusi kupatiwa mafunzo ya utengenezaji wa bomu la nyuklia.Kukamatwa kwa wanasayansi hao ni kihibitisho tosha namna Iran ilivyojiandaa kutengeneza kombora la nyuklia”

akanyamaza kidogo kisha akaendelea

“Kwa siku za hivi karibuni mzozo huu umechukua sura mpya kwa kila nchi kutishia kuishambulia nyingine.Rais wa Marekani alitishia kuisambaratisha Iran na Iran imetishia kwanza kuwashambulia washirika wa Marekani katika eneo la Mashariki ya kati na vile vile imetishia kuishambulia hadi Marekani.Iran imetoa vitisho kwamba kama Marekani itathubutu kuishambulia basi itakutana na kipigo ambacho

haijawahi kupigwa.Kauli kama hizi hatuwezi kuzipuuza na kuna taarifa za chini chini kwamba Iran ina mfumo wa kisasa wa makombora ya masafa marefu.Kwa muda mrefu sasa Marekani imekuwa ikijaribu kufanya uchunguzi kujua kuhusu silaha za Iran bila mafanikio na hii ndiyo inayoifanya Marekani kusita kuishambulia Iran kijeshi kwa kuhofia kwamba yawezekana ikawa inamiliki hizo silaha inayodai kuwa nazo na tunaweza kuwaweka katika hatari kubwa washirika wetu

walio karibu na Iran.Kwa ajili hiyo basi tumeamua kukutumia wewe katika suala hili" David akanyamaza akamtazama Mathew

"Tunataka kukutuma uende Iran kufanya kazi mbili kubwa.Kwanza ni kufanya uchunguzi kuhusiana na silaha za nchi hiyo na kazi ya pili ni kuharibu kinu kikubwa cha kurutubisha madini ya Urani" akanyamaza tena na kumtazama Mathew ambaye alikuwa kimya akimsikiliza

"Kwa nini mimi?akauliza Mathew

“Kwa nini wewe? David naye akauliza kisha akanyamaza kidogo

“Ni kwa sababu mbinu ya kutumia majasusi kuichunguza Iran imeshindwa kuzaa matunda na hadi leo hii hatujaweza kupata taarifa zozote za kuhusiana na silaha za nchi hiyo hivyo tunataka kubadili mbinu na tunataka kukupeleka wewe ambaye utapokelewa kama gaidi na shujaa bila kujua kuwa uko pale kwa kazi maalum.Iran utaingia vipi?Huu hapa mkakati wa kukuwezesha

kuingiza Iran” akasema David huku watu wote mle ndani wakiwa wamemkazia macho Mathew

“Eneo la Afrika Mashariki hivi sasa liko katika machafuko makubwa sana ya kidini.Kinachoendelea kule ni moja ya mipango yetu na kwa kuwatumia IS tumeweza kufanikisha kuibuka kwa machafuko makubwa sana ya kidini ambayo yamepelekea Marekani kupeleka vikosi vyake.Hapa unaweza ukaona ni namna gani Marekani inafaidika kutokana na

makundi ya kigaidi.Tumewatumia IS kutengeneza vurugu zile na sasa Marekani inafaidika kwa mafuta mengi kutoka Uganda.Meli za Marekani zimepanga foleni zinapishana kujaza mafuta ,akiba yetu ya mafuta inaongezeka.Hii yote ni kazi ya timu hii unayoiona humu ndani na ni mfano wa mafanikio makubwa ambayo yanapatikana kwa kuwatumia magaidi" akasema David huku akitabasamu na kumlazimu Mathew kutabasamu pia

“Kumbe hawa mabazazi ndio waliotengeneza vurugu zile Afrika Mashariki kwa ajili ya kujipatia mafuta ! Hawana huruma hata kidogo mashetani hawa.Natamani niwasambaratishe wote hapa hapa.Yaani ndugu zangu wanakufa Afrika Mashariki wao wanatabasamu kana kwamba si chochote ! Ahsante Habiba kwa kunileta hapa nimeweza kujua chanzo cha vurugu zile za nyumbani.Wamekosea sana kunieleza ukweli ! akawaza Mathew

“Safari ya kwenda Iran itaanzia Afrika Mashariki” akasema David

“Tutakutuma uende Afrika mashariki nchini Tanzania kule unakwenda kulipua ubalozi wa Marekani jijini Dar es salaam”

“Kulipua ubalozi wa Marekani? Akauliza Mathew akionekana kushangaa

“Ndiyo unakwenda kulipua ubalozi wa Marekani”

“Mnalipua ubalozi wenu wenyewe? Akauliza Mathew

“Ndiyo unakwenda kulipua ubalozi wa Marekani uliopo jjini Dar es salaam.Baada ya kulipua ubalozi huo IS watajitokeza na kudai kwamba wamehusika katika tukio hilo na tutalazimika kuongeza vikosi zaidi Afrika Mashariki kwa dhumuni la kuwasaka IS.Baada ya shambulio hilo tutaanza kukusaka kisha tutakukamata na kuitangazia dunia nzima kuwa tumemkamata mtu aliyelipua ubalozi wa Marekani jijini Dar es salaam.Tukisha kukamata

tutakupeleka mahala ambako wamehifadhiwa wanasayansi wa Iran waliotekwa wakitokea Urusi katika mafunzo ya kutengeneza bomu la nyuklia.Utakaa na wanasayansi hao na baada ya muda utasukwa mpango wa kutoroka na utawatorosha wanasayansi hao wa Iran.Kitendo hicho kitapelekea nchi ya Iran wakupokee na kukuamini kwanza watakuona shujaa kwa kulipua ubalozi wa Marekani na pili kwa kuwatorosha wanasayansi wao ambao hakuna anayefahamu

hadi leo hii wako wapi.Utaomba kupatiwa hifadhi nchini Iran na hawatakuwa na sababu yoyote ya kukunyima hifadhi na hapo ndipo utakapoanza kuifanya kazi iliyokupeleka huko” David akanyamaza akamtazama Mathew

“Si jambo jepesi ndiyo maana tulimuhitaji mtu maalum na wewe ndiye haswa unayefaa kwa kazi hii.Usihofu tutakuwezesha kwa kila kitu hadi utakapofanikiwa kuingia nchini Iran hivyo usiwe na wasi wasi” akasema David

zikapita sekunde kadhaa David akasema

“Abu Zalawi nimejitahidi sana kukupa maelezo marefu ambayo naamini umenielewa.Kuna swali lolote unataka kuuliza?

“Hapana sina swali nimewaelewa vyema” akajibu Mathew

“Vizuri sana” akasema David

“Tumejitahidi vya kutosha kukueleza kuhusu sisi na kile tunachokihitaji kwako sasa ni zamu yetu kusikia kutoka

kwako.Je unakubali kuifanya kazi hii?

Mathew hakujibu alikaa kimya kwa muda na wote mle chumbani wakamkazia macho.Akainamisha kichwa akafikiri kwa muda na kusema

“Kwanza kabisa nataka nimshukuru sana Habiba Jawad kwa kunitoa mahala nilipokuwa na kuniamini niwe msaidizi wake.Sikutegemea kama siku moja ningeweza kufika sehemu ya juu kama hii.Sikitegemea kama siku moja ningeweza kukutana na timu ya watu wenye nguvu

kubwa duniani” akasema Mathew na wale watu mle ndani wakatabasamu

“Sikuwahi kufikiri kama siku moja ningeweza kuaminiwa na kupewa jukumu kubwa kama hili nililopewa.Sina sababu yoyote ya kusema hapana.Mmenipa heshima kubwa sana ya kunituma nikafanye kazi ya taifa kubwa duniani.Ninawaahidi kwamba nimekubali na nitafanya kila mlichoniagiza nikifanye.Ninawaomba msiwe na hofu ninajiamini ninao

uwezo wa kutekeleza hiki mnachonituma nikafanye” akasema Mathew na makofi yakapigwa

DAR ES SALAAM – TANZANIA

Saa moja na dakika ishirini za jioni iliwakuta Ruby na Gosu Gosu tayari wamekwisha fika ikulu kuzungumza na Rais.Iliwalazimu kusubiri kwa saa mbili zaidi ndipo walipoonana na Rais

“Karibuni sana jamani.Mtaniwia radhi kwa

kipindi hiki mambo ni mengi mno hivyo msione kama vile nimewaweka pembeni” akasema Dr Fabian

“Usijali mheshimiwa rais tunalielewa hilo” akajibu Ruby

“Nashukuruni sana mmefika” akasema Dr Fabian na kuwachukua akina Ruby wakaelekea katika chumba cha mazungumzo

“Kwanza kabisa napenda niwashukuru mno kwa wazo zuri mlilonipa jana.Nimeona matokeo yake.Jioni hii nimepokea simu kutoka kwa Mufti wa Tanzania akaniomba

tukutane tuzungumze na akashauri kama ikiwezekana tukutanishwe viongozi wote wa kuu wa dini tukae meza moja tuzungumze tuone namna tutakavyoweza kutoka katika janga hili linalotukabili hivi sasa.Nimekubali wazo lake na tayari nimewaelekeza wasaidizi wangu wanisaidie kuwatafuta viongozi wengine wa dini upande wa wakristu ili tuandae mkutano wa pamoja tuzungumze.Masuala haya yanayohusiana na imani za dini hayawezi kumalizwa na vikosi vya jeshi bali kwa

mazungumzo na viongozi wa dini ambao wanayo nguvu ya kuwashawishi waumini wao kuacha vurugu.Nashukurusana kwani ni wazo lenu ndiyo limezaa haya mazungumzo.Nimepokea pia taarifa kutoka kwa mkuu wa jeshi la polisi ameniambia kwamba kwa siku ya leo vurugu zimepungua tofauti na siku ya jana.Wote wanaamini hotuba ile imesaidia sana kwa vurugu kupungua.Hapo pia ninaelekeza shukrani zangu kwenu kwani sikuwa na wazo

lile la kuhutubia taifa” akasema Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais hata sisi tunashukuru sana kama wazo lile limezaa matunda.Tuna imani kikao hicho cha viongozi wakuu wa dini mbali mbali kitakuwa na matunda mazuri” akasema Ruby

“Naamini hivyo.Tunaweza kufikia muafaka mzuri.Vipi kwa upande wenu kuna chochote mmekipata?

“Mheshimiwa Rais tumeanza kulifanyia kazi lile suala la kumchunguza Karim

Abdallah.Tumefika nyumbani kwake lakini tumemkosa na inaonekaana aliondoka haraka haraka yeye na familia yake.Katika uchunguzi wetu tulipata orodha ya watu kadhaa ambao aliwasiliana nao na mtu wa mwisho kuwasiliana naye alikuwa jijini Tanga.Tuliwatumia watu wetu wa kule Tanga kumfuatilia huyo mtu lakini walikuta nyumba yake ikiwa imeteketea kwa moto.Tulimchunguza tena huyo jamaa na kumfuatilia mtu ambaye aliwasiliana naye mara ya mwisho ambaye naye

alikuwa hapo hapo Tanga na watu wetu walipoingia katika hiyo nyumba walikuta kuna maiti ya mwanamke amechomwa kisu kifuani” akasema Ruby na kumuonyesha Rais picha za Yule mwanamke

“Huu ni unyama mkubwa sana” akasema Dr Fabian

“Watu wetu walichukua alama za vidole katika mpini wa kisu wakazituma kwetu kwa ajili ya kuzifanyia kazi na tukamfahamu mtu aliyefanya kitendo kile ni mumewe ambaye ni mchungaji anaitwa

Augustin Kawala.Huyu naye hajulikani mahala alipo.Ukifuatilia kuanzia kwa Karim hadi kwa huyu Augustin wana mambo yanayofanana,wote wamewasiliana ndani ya siku moja na simu zao zimezimwa siku moja halafu wote hawapatikani tena na hawajulikani wako wapi.Hii inatufanya tuamini yawezekana wakawa kitu kimoja”

“Dah ! akasema Dr Fabian

“Hatukuishia hapo.Baada ya kuwakosa hao watu

tuliokuwa tunawatafuta tuliendelea kumchunguza Karim na tukafuatilia mawasiliano yake ya wiki moja kabla ya vurugu kuanza na tukagundua kwamba amewasiliana mara ishirini na tatu na mtu mmoja anaitwa Joshua Lulangwa ambaye ni mwanasiasa wa chama cha upinzani nchini Uganda.Mheshimiwa Rais hapo ndipo tulipofikia na kukwama.Tunataka kumchunguza huyu mwanasiasa Joshua Lulangwa tufahamu mahusiano yake na

Karim Abdallah.Wamewasiliana mara nyingi zaidi ndani ya wiki moja kabla ya vurugu kuanza.Tumekuja hapa kuomba msaada wako ili uweze kuzungumza na rais wa mpito wa Uganda Jenerali Paul Mukasa kumuomba atusaidie tuweze kupata taarifa za Joshua Lulangwa" akasema Ruby

"Ruby kwanza kabisa nataka niwapongeze kwa namna mnavyojituma katika kutafuta mzizi wa jambo hili.Mimi nitawasiliana na

Jenerali Paul kumuomba atusaidie kupata taarifa za huyo mtu ambaye amekuwa na mawasiliano na Karim Abdallah.Ninaamini hadi kufika kesho jioni tutakuwa tumepata taarifa zake”

“Ahsante sana mheshimiwa Rais”

“Kuna lingine la kuzungumza?Nina kikao kingine muda si mrefu” akasema Dr Fabian

“Ni hilo tu mheshimiwa rais lililotuleta hapa kwako jioni ya leo”

“Basi nawashukuruni.Endeleeni na jitihada za kuhakikisha tunaupata mzizi wa jambo hili.Kama kuna chochote mnakihitaji nijulisheni mara moja” akasema Dr Fabian na kuagana na akina Ruby.

Baada ya akina Ruby kuondoka Dr Fabian akaelekea chumbani kwake na kuketi sofani akashusha pumzi.Akachukua simu na kuzitafuta namba za simu za Jenerali Paul Mukasa akampigia

“Dr Fabian” akasema Jenerali Mukasa

“Jenerali Mukasa.Habari za huko?

“Huku bado hali si shwari.Vurugu zinaendelea kupamba moto kila uchao.Kadiri siku zinavyozidi kwenda upepo wa vurugu hizi unabadilika na sasa kunaanza kuibuka makundi yenye silaha ambayo yanashambuliana na vikosi vya jeshi.Tunaendelea kuvichunguza vikundi hivi vinatoka wapi na silaha vinatoa wapi.Machafuko haya yanabadilika kutoka katika

machafuko ya kidini na sasa yanaelekea kwenye uasi.Hivi vikundi vilivyoibuka vinazidi kuifanya hali ya amani kuwa tete zaidi kwani vina silaha nzito” akasema Jenerali Paul Mukasa

“Hilo limeanza kujitokeza hata huku Tanzania.Kumeibuka makundi ambayo siyo ya kidini yanavunja nyumba,maduka makubwa na kupora.Wanaharibu na kuchoma majengo ya serikali na wana silaha.Nimeelekeza tuwachunguze makundi hayo

tujue yametokeaje na nini hasa malengo yake.Jana nimeelekeza mawasiliano ya simu yarejeshwe hapa Tanzania na nikalihutubia taifa nikawataka watu watafakari na kuachana na vurugu hizi zinazoendelea.Nimefurahi kumekuwa na maendeleo mazuri kwani taarifa niliyoipata jioni hii ni kwamba machafuko yameanza kupungua na kesho nitakuwa na kikao na viongozi wa dini halafu tutajadili kuhusiana na vurugu hizi”

“Mheshimiwa Rais hizo ni dalili nzuri za kuelekea katika suluhu ya vurugu hizi” akasema Jenerali Mukasa

“Jenerali Mukasa nimekupigia kuna jambo ninataka tulijadili kidogo.Unahisi nini hasa chanzo cha vurugu hizi ambazo zimeanzia Uganda na kusambaa hadi Tanzania na Kenya? Akauliza Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais,kwa kweli hata mimi nashindwa kuelewa namna vurugu hizi zilivyoanza.Zilianza kiajabu ajabu sana na kushika kasi

kama moto wa petrol.Mpaka sasa tumeelekeza nguvu katika kuzimaliza na hatujajikita bado kujua chanzo chake” akasema Jenerali Paul Mukasa

“Ipo timu hapa Tanzania ambayo nimeipa kazi ya kuchunguza chanzo cha vurugu hizi kwa upande wa Tanzania.Katika uchunguzi wao wa awali wamebaini kuna mtu mmoja ni mwanasiasa ambaye wakati kukiwa na vugu vugu la machafuko hapa Tanzania aliandika ujumbe katika ukurasa wake wa twitter akiwataka waumini wa dini ya

kiislamu wakawashambulie watu wa dini nyingine.Tunahisi huyu anaweza akawa anahusiana kwa namna Fulani na machafuko haya.Tunahisi vile vile kwamba machafuko haya yana chembe chembe za kisiasa ndani yake.Tumechunguza watu kadhaa ambao wana mahusiano na huyo mwanasisasa lakini wote wametoweka na simu zao hazipatikani tena.Inaonekana huu ni mtandao mmoja.Katika uchunguzi wao wamegundua

kwamba Karim alikuwa na mawasiliano na mwanasiasa mmoja wa Uganda anaitwa Joshua Lulangwa.Karim na Joshua wamewasiliana mara nyingi zaidi katika wiki moja kabla ya machafuko kuanza.Tunataka kumchunguza Joshua kufahamu mahusiano yake na Karim na kisha tujue kama wana mahusiano yoyote na vurugu hizi zinazoendelea.Tunaomba msaada wako kupata taarifa za huyu mtu" akasema Dr Fabian

“Hakuna tatizo mheshimiwa Rais nitawaelekeza watu wangu wafanye uchunguzi kuhusiana na huyo mtu kisha nitakujulisha”

“Nashukuru sana Jenerali Mukasa” akajibu Dr Fabian na kukata simu

“Naanza kukubaliana na Ruby kwamba yawezekana machafuko haya yana chembe chembe za kisiasa ndani yake.Lazima tuhakikishe kwa gharama zozote wale wote waliosababisha machafuko

haya wanapatikana ”
akaendelea kuwaza Dr Fabian

WASHINGTON DC –
MAREKANI

“Mama Habiba siamini kwa hiki ulichonifanyia.Hii ndiyo misheni kubwa uliyoniambia kwamba unaniandalia? Akauliza Mathew Mulumbi baada ya kupewa dakika chache kuagana na Habiba kabla ya kwenda kujiandaa kutekeleza jukumu kubwa alilopewa.

“Ndiyo Mathew” akajibu Habiba Jawad

“Siamini mama kama umekuja kuniuza kwa hawa jamaa ambao sasa wananituma nikafanye kazi zao za hatari.Kwa nini umenifanyia hivi mama Habiba? Akauliza Mathew

“Mathew sikiliza hatuna muda mrefu wa kuongea.Nimekuleta hapa kwa makusudi kabisa.Kama kweli una nia ya dhati ya kumaliza ugaidi duniani basi hii ndiyo nafasi pekee unayopaswa kuitumia.Hiki kitengo ndicho

kinachoongoza makundi karibu mengi ya kigaidi duniani hivyo umefika sehemu unakotakiwa ufike.Finish them.Fanya wanachokutuma ufanye wachunguze vizuri halafu mwisho wa siku wamalize.Kikundi hiki ni hatari sana kwa mustakabali wa dunia.Hakikisha ……" akasema Habiba na kugeuka baada ya kusikia hatua za mtu akiwafuata ambaye alitumwa kumchukua Mathew.Habiba akamtaka mtu Yule kusubiri dakika mbili

“Mathew hakikisha unafanikisha malengo yako.Ifanye dunia ikukumbuke kwa vizazi na vizazi.Maliza kundi la kigaidi la IS na makundi mengine.Kisafishe kikundi hiki kidogo cha watu hawa ambacho ndicho kinachohatarisha amani ya dunia.Hii ni misheni kubwa na ya hatari.Lolote linaweza kutokea katika misheni hii mimi ninakuombea uimalize salama na kila pale nitakapokuwa na uwezo wa kukusaidia nitafanya hivyo.Jambo la mwisho baada

ya kumaliza misheni hii kama utakuwa salama tafadhali usirejee tena Riyadh.Nenda nyumbani kaendelee na maisha yako.Kaungane tena na familia yako kwani lengo lako litakuwa limetimia kuhusu kupambana na ugaidi.Kuhusu Najma usiwe na hofu nitazungumza naye na ataelewa.Narudia tena usirejee Saudi Arabia kwani hadi wakati huo sintakuwepo tena.Ule utajiri wako wote niliokupa utaendelea kuwa wako na fedha zote zitawekwa katika ile akaunti yako

utakapomaliza misheni hii utatulia na familia yako na kufurahia utajiri huo.” akasema Habiba Jawad ambaye machozi yalikuwa yanamtiririka

“Mathew hii naamini itakuwa ni mara ya mwisho kwa mimi na wewe kuonana hapa duniani.Kwa sasa nina amani na ninaamini hata nikifa leo nimeacha chuma ambacho hakishiki kutu ambacho kitamaliza ugaidi.Nakutakia kila la heri” akasema Habiba na kumkumbatia Mathew halafu

akaanza kuondoka huku Mathew naye akiwa amesimama akimtazama.

“Ahsante Habiba Jawad kwa kunifikisha hapa.Umefanya jambo kubwa sana kunifikisha hatua hii na sintakuangusha” akawaza Mathew akiwa bado amesimama akimtazama Habiba akiingia katika lifti na mlango ukajifunga

Mathew aliongozana na Yule mtu aliyetumwa kumchukua hadi katika gari wakaondoka.Ilikuwa ni safari ya kimya kimya na Mathew

hakujua alikokuwa anapelekwa.

Safari yao iliishia katika nyumba moja ambayo geti lake lilikuwa wazi wakaingia ndani.Yule jamaa akashuka garini na kumtaka Mathew ashuke kisha wakaingia ndani ya ile nyumba ambako walimkuta jamaa mmoja mnene aliyekuwa sebuleni akitazama runinga.Alikuwa kifua wazi na alikuwa amevaa kaptura ya rangi za jeshi.Akawakaribisha na Yule jamaa aliyemleta Mathew katika nyumba ile akatoka nje

akawaacha Mathew na yule jamaa

“Jina lako nani? Akauliza Yule jamaa akiwa ameyaelekeza macho yake katika mecho ya mpira wa kikapu iliyokuwa inaendelea runingani

“Abu Zalawi” Mathew akajibu

“Naitwa Peter Tylor.Karibu” akasema Peter huku akiinua kikombe cha kahawa na kunywa

“Ahsante” akajibu Mathew.Peter akanywa kahawa halafu akaweka

kikombe mezani akazima runinga na kumtazama Mathew

“Umewahi kuishi Afrika? Akauliza Peter Tylor

“Ndiyo nimewahi kuishi Nairobi Kenya na Cairo” akajibu Mathew

“Vizuri.Unakwenda tena Afrika lakini safari hii unakwenda Tanzania.Utaondoka hapa na ndege ya jesi kuelekea Tanzania.Utakapofika Dar es salaam utafikia katika kambi ya wanajeshi wa Marekani na atakuja mtu Fulani anaitwa

Assad Ismail kukuchukua.Huyu tayari ana maelekezo yote ya kuhusu wewe na ndiye atakayekusaidia kufanikisha kazi uliyotumwa kuifanya hapo Dar es salaam.” akasema Peter Tylor na kumchukua Mathew katika chumba kimoja akaanza kumpa maelekezo ya kazi ambayo anatakiwa kwenda kuifanya Dar es salaam.Baada ya kupewa maelekezo yote Mathew na Yule jamaa wakaingia garini na kuondoka kuelekea katika uwanja wa

ndege wa kijeshi ambako kulikuwa na ndege inamsubiri.

“Safari njema” akasema Peter na Mathew akaingia katika ndege ile ya jeshi ambayo haikuchukua muda ikapaa kuelekea Tanzania.

“Habiba amenifikisha mahala ambako sikutegemea kufika.Nimegundua siri kubwa sana ambayo dunia haiijui.Nimekutana na kikundi cha watu wachache wenye nguvu ambao wanaamua kitu gani wafanye katika nchi gani hapa duniani.Machafuko yanayoendea Afrika mashariki

kumbe ni mipango ya Marekani kutaka kuchukua mafuta ya Uganda.Hawajali mamia ya watu wanaouana kila uchao wao wanachokitazama ni maslahi yao tu.Hawa ni watu wakatili sana ! akawaza

“Namshukuru sana Habiba Jawad kwa kunifikisha hapa.Aliponiambia kwamba kuna mambo mengi ambayo siyafahamu bado alikuwa sahihi.Kuna mambo sikuwa nikiyafahamu na mojwapo ni hili la idara maalum ndani ya shirika la ujasusi la marekani

CIA kushirikiana na makundi ya kigaidi kwa ajili ya maslahi ya Marekani” akawaza Mathew

“Ninakwenda kufanya kazi ya kigaidi.Kutoka ujasusi hadi ugaidi ! akaendelea kuwaza Mathew akiwa ameinamisha kichwa

“Nitafanya wanavyotaka lakini hawataamini kwa kile nitakachowafanyia.Ile idara ndogo katika CIA lazima niifuilie mbali,lazima dunia ifahamu kile ambacho watu hawa wanakifanya.Katika hili natakiwa kuwa mvumilivu.Natakiwa kwanza

kujenga imani kwao ili waniamini na ndipo nitakapoweza kutekeleza mipango yangu.Lakini nasikitika sana pale dunia nzima watakapojua mimi ni gaidi na nimelipua ubalozi wa Marekani jijini Dar es salaam.Ruby ataumia sana akisikia jambo kama hili.Wenzangu akina Gosu Gosu na Austin hawataamini macho yao pale watakaposikia kwamba mimi ndiye niliyelipua ubalozi wa Marekani.Watoto wangu watapatwa na mstuko mkubwa

baada ya picha zangu kutolewa kwamba ndiye niliyelipua ubalozi wa Marekani na nitatajwa kama gaidi.Jina langu litachafuka.Watu wanaonifahamu hawataamini kama kweli nimegeuka kutoka jasusi hadi gaidi.Lakini baada ya kuchafuka kwa kujulikana kama gaidi mwisho wa mchezo huu dunia nzima itanisifu kwa kile nitakachokifanya.Halafu ! akawaza Mathew na kuinua kichwa baada ya mmoja wa wanajeshi waliokuwamo mle ndegeni kumgusa na kumpatia chupa ya bia.

“Ahsante” akasema Mathew na kunywa funda moja

“Marekani hawajui kama mimi ni mtanzania.Hawajui kama mimi ni jasusi na jina langu ni Mathew Mulumbi na si Abu Zalawi kama walivyoambiwa na Habiba Jawad.Baada ya picha zangu kusambaa duniani kwamba mimi ndiye niliyelipua ubalozi wa Marekani jijini Dar es salaam lazima siri itafichuka kwamba mimi ni mtanzania na nitakuwa nimejiweka katika matatizo mimi na hata Habiba

pia ambaye amewahakikishia wamarekani kuwa mimi ni raia wa Saudi Arabia.Lakini hii haiwezi kunizuia kuendelea na mipango yangu.Dunia itatikisika.Kila chombo cha habari duniani lazima kitaniongelea mimi” akaendelea kuwaza Mathew huku ndege ikiendelea kupasua anga kuelekea Tanzania

RIYADH – SAUDI ARABIA

Saa nane za mchana Habiba Jawad aliwasili jijini Riyad Saudi Arabia akitokea Washington DC Marekani.Katika uwanja wa ndege alipokewa na mwanae Najma ambaye alistushwa kwa Habiba kurejea peke yake bila ya Mathew Mulumbi.

“Mbona umerejea peke yako mama,Abu yuko wapi?akauliza Najma

“Tutazungumza tukifika nyumbani Najma” akasema Habiba na safari ikaendelea kimya kimya

Waliwasili nyumbani kwa Habiba na Najma hakutaka kupoteza muda akamtaka mama yake wazungumze.

“Mama nafahamu umechoka sana kwa safari ndefu.Takribani saa kumi na nne umekuwa angani ukisafiri lakini naomba tafadhali unipe dakika chache tuzungumze.Nina jambo ambalo haliwezi kusubiri na nilitamani nikufuate huko huko Marekani tulizungumze” akasema Najma na Habiba akamtazama mwanae

akagundua kweli kuna kitu kinamsumbua

“Kitu gani kinakusumbua Najma?Ni kuhusu kutokurudi na Abu Zalawi?akauliza Habiba

“Hilo ni moja wapo lakini kuna lingine kubwa zaidi ya hilo” akajibu Najma

“Nieleze tafadhali”

“Kabla sijakueleza chochote mama nataka unihakikishie kwamba utanieleza ukweli mtupu kwa kile nitakachokuuliza” akasema Najma.Habiba akamtazama halafu akasema

“Nini kinakusumbua Najma? Niambie kile kinachokusumbua na mimi nitakujibu” akasema Habiba

“Mama nataka unieleze kila kitu kuhusiana na Abu Zalawi”

“Abu Zalawi ni mume wako,wewe ndiye uko naye karibu zaidi na ni wewe unayetakiwa kumfahamu vyema.Hukupaswa kuniuliza mimi kuhusu Abu Zalawi kwani tayari umekuwa naye kwa muda wa miezi kadhaa hivi sasa.Unapaswa tayari uwe

unamfahamu vyema” akasema Najma

“Mama nakuomba tafadhali unieleze ukweli kuhusiana na Abu Zalawi.Ni nani huyu mtu? Umemfahamuje? Akauliza Najma

“Najma nini hasa kinachokufanya uniulize mimi habari za Abu Zalawi?

“Mama nakuomba sana unisaidie kunieleza kuhusiana na huyu mtu nahitaji sana kumfahamu.Wewe ndiye unayemfahamu vyema kuliko mimi.Naomba tafadhali

unieleze kila kitu unachokifahamu kuhusu Abu Zalawi” akasema Najma

“Najma unanishangaza.Kuna nini kati yako na Abu Zalawi? Kuna mgogoro wowote kati yenu? Niambie tafadhali kama kuna tatizo lolote” akasema Habiba

“Mama ngoja nikuweke wazi ili upate picha halisi ya mzigo ninaoubeba.Ulinitaka niolewe na Abu Zalawi ambaye ulidai ni mwanaume ambaye ananifaa.Nilitokea kumpenda Abu Zalawi kabla hata sijamtia machoni kufuatia maelezo

yako na nilipomuona kwa macho nilimpenda na nikakubali kuolewa naye na ninakiri kwako mama kwamba ninampenda sana Abu Zalawi lakini kuna mambo yamejitokeza ambayo yamenifanya nitake kumfahamu vyema huyu mtu ni nani?”

“Nini kimetokea Najma? Akauliza Habiba

“Kabla ya safari ya kwenda Marekani ulizungumza na Abu Zalawi na aliporejea chumbani alionekana kama vile amechanganyikiwa.Sifahamu

ni kitu gani ulimweleza lakini hakuwa Yule niliyemzoea.Alichukua kitabu hiki hapa akakifungua akatafuta namba za simu ambazo zina jina la Ruby akapiga zaidi ya mara tatu lakini simu ya huyo mtu haikuwa ikipatikana.Wakati akiendelea kumtafuta huyo Ruby nilikichukua kitabu hiki na kuzikuta namba hizo za Ruby.Nilimuuliza Ruby ni nani akastuka sana na kuninyang'anya kile kitabu.Mama mimi nina wivu sana na ndiyo maana sikutaka

kujiingiza katika masuala ya mapenzi kwa kuhofia kuumizwa. Mlipokwenda Marekani nilipiga zile namba za Ruby alizopiga Abu Zalawi akapokea mwanamke ambaye yuko Tanzania lakini aligoma kunitajia jina lake.Nilimuuliza kama anamfahamu Abu Zalawi akakana kumfahamu,alikana kuwa na rafiki au mtu anayemfahamu mwenye jina la Abu Zalawi.Baadae akanipigia simu akanitaka nimtumie picha ya Abu Zalawi na hapo ndipo kilipotokea kizaa zaa”

Najma akanyamaza kidogo halafu akasema

“Kwa muda wa miezi mitatu tumekuwa tukizunguka sehemu mbali mbali duniani tukifanya utalii.Katika safari yetu hiyo tulipiga picha nyingi sana lakini kitu cha ajabu ni kwamba nilipozitafuta picha tulizopiga mimi na Abu katika safari yetu sikupata hata picha moja.Nilihifadhi picha nyingi katika kompyuta yangu nyingine zilikuwepo katika kamera na hata katika simu yangu lakini huko kote hakukuwa na picha hata

moja.Hiki kitu kimenishangaza sana mama namna picha zilivyotoweka.Hakuna mtu yeyote aliyeingia chumbani kwetu zaidi yetu sisi hivyo naamini aliyefuta picha hizo lazima atakuwa Abu Zalawi.Nimejiuliza maswali mengi kwa nini akafuta picha zetu?Nimeshindwa kupata jibu ndiyo maana nataka unieleze kuhusiana na huyu mtu ni wa aina gani? Tafadhali mama” akasema Najma na Habiba akavuta pumzi ndefu

“Mambo yamekwisha haribika.Tayari Najma amekwisha hisi kitu kuhusu Abu zalawi.Nadhani ni wakati wake wa kuufahamu ukweli” akawaza Habiba

“Najma kuna jambo ambalo nataka nikueleze kuhusu Abu Zalawi.Kwanza kabisa ni kwamba Abu Zalawi hatarejea tena.Ameondoka” akasema Habiba na sura ya Najma ikabadilika

“Unasemaje mama ?! akauliza Najma

“Najma Abu Zalawi hatarejea tena.Ameondoka”

“Mama sijakuelewa”

“Najma kuna mambo mengi ambayo huyafahamu kuhusu mimi” akasema Habiba na kumtazama Najma ambaye alionekana kuchanganyikiwa

“Maisha yangu yamejaa siri nyingi ambazo nyingine nitakueleza lakini nyingine nitakwenda nazo kaburini.Nina sababu yangu ya kufanya hivyo” akasema Habiba na kunyamaza tena akamtazama Najma

“Siri ya kwanza ni kuhusu huu utajiri wangu.Utajiri

wangu huu ambao ninautumia katika kufadhili makundi mbali mbali ya kigaidi niliurithi kwa baba yake Abu Dahir lakini naye utajiri huu hakuupata hivi hivi.Leo nitakupa siri ya huu utajiri wangu" akasema Habiba na kunyamaza akamtazama Najma

"Asili ya utajiri wangu huu ni Marekani.Wao ndio waliomuwezesha baba yake Abu Dahir na alipofariki mimi ndiye niliyerithi utajiri huo.Kwa nini Marekani walimpa utajiri huu mkubwa?

Akauliza Habiba lakini Najma hakujibu kitu chochote

“Ndani ya shirika la ujasusi la Marekani CIA kuna kitengo ambacho kinajishughulisha na mashirikiano na makundi ya magaidi.Kitengo hiki ndicho kilichotuwezesha kuwa na utajiri huu mkubwa na lengo kuu la kutupa utajiri huu ni kwa ajili ya kuyafadhili makundi ya kigaidi katika operesheni zao mbali mbali zenye maslahi kwa Marekani hivyo basi kwa muda huu wote nimekuwa nikifanya kazi na

Marekani.Ufadhili huu ambao tumekuwa tukiwapa makundi ya magaidi ni maelekezo ya Marekani” Sura ya Najma ilibadilika alifungua mdomo wake akataka kusema kitu lakini maneno hayakutoka

“Nimekustua Najma.Lakini umefika wakati wa wewe kufahamu kila kitu.Nimeamua kukushirikisha siri chache kuhusu mimi” akasema Habiba

“Nimefanya kazi na Marekani kwa muda mrefu na sasa nimechoka.Sitaki kuendelea tena kuwa mfadhili

wa makundi ya kigaidi ndiyo maana nikamleta Abu Zalawi ili aweze kulimaliza jambo hili.Kuna mambo ambayo huyafahamu kuhusu Abu Zalawi na leo nitakufahamisha”Habiba akanyamaza kidogo halafu akasema

“Abu Zalawi jina lake halisi anaitwa Mathew Mulumbi ni mtanzania”

“Mungu wangu ! akasema Najma.Habiba akaendelea

“Abu Zalawi si gaidi kama nilivyokufahamisha awali bali ni jasusi”

“Jasusi ? ! Najma akashangaa

“Ndiyo ni jasusi.Najma kuna mengi ambayo ningetaka kukueleza lakini nitazungumza nawe siku nyingine hayo machache yanatosha kwa leo.Kubwa ambalo nataka ulifahamu ni kwamba Abu Zalawi au Mathew alikuwa hapa kwa ajili ya kazi maalum na sasa wakati wake umefika wa kwenda kutekeleza majukumu yake na kazi hiyo anayokwenda kuifanya ni kwa ajili ya usalama wenu wewe na kaka yako.Abu ndie mkombozi

wenu kwani akifanikiwa katika misheni hiyo itakuwa ni salama yenu lakini akishindwa maisha yetu yatakuwa shakani.Abu Zalawi hatarudi tena”

“Unamaanisha nini mama?

“Misheni anayokwenda kuifanya ni misheni ya hatari kubwa sana na uhakika wa kurudi salama katika misheni hiyo ni mdogo” akasema Habiba

“Mama kwa nini ukanifanyia hivi? Kwa nini ukanitaka niolewe na Abu

Zalawi wakati ukijua ni mtu wa namna gani?Kwa nini ukaniacha nikazama mapenzini na Abu Zalawi halafu unamuondoa? Akauliza Najma

“Nilikuwa na sababu zangu kukutaka uolewe na Abu Zalawi.Bila kuolewa naye asingekubali kukaa nasi hapa kwa ajili ya misheni ambayo nimemtuma akaifanye.Amekaa nasi hapa hadi ulipofika muda wake wa kuondoka kwa sababu yako”akasema Habiba

“Mama wewe ni shetani.Una roho ya kishetani !

Huna ubinadamu hata kidogo.Mama wewe ni mkatil……” Akasema Najma na Habiba akamnasa kofi

“Haya yote niliyoyafaya ni kwa sababu yenu.Nafanya kila hatua kuwalindeni ili muwe salama vinginevyo ninyi nyote hivi sasa mngekwishauawa.Kuanzia sasa anza kuzoea hali hii.Abu Zalawi ana mke wake na watoto hawezi kurudi tena.Kumpoteza Abu si mwisho wa mais…”akasema

Habiba na Najma akatoka mbio huku akilia.

“Nimemuumiza sana Najma.Sikutaka aufahamu ukweli hu lakini kwa hatua aliyokuwa ameifikia ni lazima aufahamu ukweli.Itamchukua muda mrefu kukubaliana na ukweli h….” Habiba akastuka baada ya mmoja wa walinzi wake kuingia mle ndani akikimbia

“Kuna nini ?akauliza Habiba kwa wasi wasi.

“Mama umesikika mlio wa risasi katika nyumba ya Abu Zalawi ! akasema Yule mlinzi

na Habiba akatoka mbio akiongozana na Yule mlinzi na kukuta walinzi wengine tayari wamekwisha fika katika nyumba ile ya Mathew.Habiba akiwa na wale walinzi wakaenda chumbani kwa Najma walinzi wakavunja mlango akaingia ndani.Najma alikuwa amelala katika dimbwi la damu.Hakuwa na uhai tena.Alijipiga risasi ya kichwa.Habiba akaanguka na kupoteza fahamu.

MPENZI MSOMAJI USIKOSE SEHEMU IJAYO.....